WILLIAM
SHAKESPEARE

Juliasi Kaizari

kimetafsiriwa na

JULIUS K. NYERERE

WILLIAM SHAKESPEARE

JULIASI KAIZARI

kimetafsiriwa na

JULIUS K. NYERERE

Nairobi
OXFORD UNIVERSITY PRESS
Dar es Salaam

Oxford University Press
OXFORD LONDON GLASGOW
NEW YORK TORONTO MELBOURNE AUCKLAND
NAIROBI DAR ES SALAAM CAPE TOWN
KUALA LUMPUR SINGAPORE HONG KONG TOKYO
DELHI BOMBAY CALCUTTA MADRAS KARACHI

and associates in
BEIRUT BERLIN IBADAN MEXICO CITY NICOSIA

ISBN 0 19 572169 1
© OXFORD UNIVERSITY PRESS 1963,
OXFORD is a trademark of Oxford University Press

This Revised Edition, 1969
Reprinted 1969, 1971, 1974, 1975, 1984, 1985

Mchezo huu unalindwa na Sheria ya Haki ya Kunakili; na kila ombi la kutolea hadharani (ila kutoka kwa vyuo, ambavyo vyote vinaruhusiwa kuutolea bure) lazima lipelekwe
Oxford University Press
P.O. Box 72532
Nairobi

Sura ya mbele imechorwa na
SEFANIA TUNGINIE

Published by Oxford University Press, East and Central Africa, Science House, Monrovia Street, P.O. Box 72532, Nairobi and printed by Acme Press (K) Ltd., P.O. Box 40497, Mfangano Street, Nairobi, Kenya

FAHARISI

Utangulizi	vi
Waliomo katika mchezo	viii
Kitendo cha kwanza	
Onyesho la kwanza	1
Onyesho la pili	3
Onyesho la tatu	14
Kitendo cha pili	
Onyesho la kwanza	20
Onyesho la pili	31
Onyesho la tatu	35
Onyesho la nne	36
Kitendo cha tatu	
Onyesho la kwanza	38
Onyesho la pili	48
Onyesho la tatu	58
Kitendo cha nne	
Onyesho la kwanza	60
Onyesho la pili	62
Onyesho la tatu	64
Kitendo cha tano	
Onyesho la kwanza	76
Onyesho la pili	80
Onyesho la tatu	81
Onyesho la nne	85
Onyesho la tano	86

UTANGULIZI WA TOLEO LA PILI

Toleo hili ni tofauti na toleo la kwanza. Toleo hili lina mabadiliko na masahihisho mbalimbali. Badiliko kubwa ni la majina. Katika toleo la kwanza nilisema kuwa taabu moja katika kuhesabu mizani ilikuwa ni kujua kama 'Brutus' ni 'Burutusi' au 'Brutusi'. Ili kuondoa shida hiyo nimejitahidi kuyabadili majina yote ili matamshi yake yafanane na matamshi ya Kibantu. Kwa hiyo tangu sasa mchezo huu si 'Julius Caezar', bàli ni 'Juliasi Kaizari'! Jamaa waliomo humu wamekuwa OTTAVIO KAIZARI, MARIKO ANTONIO, MARIKO BURUTO, SISERO, KAPUNIA, POSHIA na kadhalika. Mimi nimekwisha kuyazoea majina haya, natumaini kuwa na ninyi pia mtayazoea.

Mabadiliko mengine yametokana na badiliko hilo kubwa la kubadili majina. Ni dhahiri kwamba mstari ambao ulikuwa na 'Caèzar' ('Siza') yaani mapigo mawili, lazima ubadilishwe ikiwa sasa utakuwa na 'Kaizari', mapigo manne.

ANTONIO mahali pengine ni Antoni. Hii ni kwa sababu ya mizani. Sikutumia uhuru huu mara nyingi. Lakini kwa 'Antonio' na 'Antoni' nilifikiri ninacho kisingizio kizuri sana cha kufanya hivyo; na kisingizio hicho ni kwamba Shakespeare mwenyewe hutumia 'Antonius' na katika kueleza tofauti baina yake na Kasio anasema, '*He loves no plays, as thou dost, Antony.*'

Nimetumia nafasi ya mabadiliko haya pia kusahihisha makosa fulani yaliyokuwamo katika toleo la kwanza. Makosa haya yalikuwa ya aina mbalimbali. Pengine nilikuwa nimekosea tafsiri yenyewe; pengine mistari fulani ilikuwa imeachwa; na pengine kulikuwa na makosa ya kupiga chapa. Jamaa wengi wamenisaidia kugundua makosa hayo na ningependa kuchukua nafasi hii kuwashukuru.

Kwanza nawashukuru Mabwana Lyndon Harries na marehemu Amri Abedi kwa majadiliano yao ya kibingwa juu ya tafsiri yangu ya kwanza. Majadiliano hayo yamenisaidia sana. Matumaini yangu ni kwamba yamewasaidia wengine pia kujishughulisha na ufasaha wa Kiswahili. Pia nawashukuru Bibi Josephine Snaith wa University College, Dar es Salaam; Bwana John Allen wa Makerere College, Uganda, na Bwana Valentine Ostrovsky, mwandishi wa Gazeti la Literaturnaya Gazeti la Moscow, U.S.S.R. Masahihisho mbalimbali yametokana na Bibi Snaith ambaye pamoja na hayo kaisoma tena tafsiri yangu ya pili zaidi ya mara moja kabla ya kupelekwa kwa

wachapaji; na pia kaisoma baada ya kupigwa chapa ili kuondoa makosa ya uchapaji. Wazo la kubadili majina nililipata baada ya kusoma uhakiki wa Bwana John Allen juu ya tafsiri yangu ya kwanza. Nadhani Bwana Allen kaisifu mno tafsiri yangu, lakini napenda kumshukuru hasa kwa kuwajibu watu wasiojua Kiswahili, ambao wanafikiri kuwa Kiswahili si lugha pana ya kutosha kueleza mawazo makubwa au ufasaha safi bila kuazima mno maneno mapya ya kigeni. Namshukuru sana Bwana Valentine Ostrovsky. Bila shaka kwake yeye, lugha zote mbili, Kiswahili na Kiingereza, kajifunza: na ni bingwa wa zote. Kiswahili kajifunza mwenyewe, kitabuni, bila kufika Afrika.

Nawashukuru pia Mabwana Bernth Lindfors na Morris Goodman wa Los Angeles, U.S.A., kwa maswali yao ambayo yamenisaidia kuona makosa fulani na kuyasahihisha. Namshukuru Bwana M. Shekalaghe, ambaye kwa wema wake alinipigia taipu maandiko yangu kabla ya kupelekwa kwa wapiga chapa. Na mwisho kabisa ningependa kuwashukuru sana vijana wa St. Francis College, Pugu, pamoja na waalimu wao kwa kucheza mchezo wenyewe katika jukwaa. Pengine wao wenyewe hawatambui jinsi walivyoucheza vizuri. Bibi mkubwa wangu alikuwa miongoni mwa watazamaji. Baada ya nusu ya kwanza aliondoka asirudi tena. Baadaye tulipomwuliza kwa nini hakurudi alituambia kwamba alihuzunishwa sana na kifo cha Juliasi Kaizari, ndiyo maana hakupenda kuendelea kuuona. Ni dhahiri kuwa ulichezwa vizuri!

Dar es Salaam 1968 JULIUS K. NYERERE

WALIOMO KATIKA MCHEZO

JULIASI KAIZARI	
OTTAVIO KAIZARI MARIKO ANTONIO M. EMILIO LEPIDO	Wakuu watatu waliotawala kwa sharika baada ya kifo cha Juliasi Kaizari
SISERO PUBULIO POPILIO LENA	Maseneta
MARIKO BURUTO KASIO KASIKA TIREBONIO LIGARIO DESIO BURUTO METELLO SIMBER SINNA	Mahaini waliofanya njama ya kumwua Kaizari
FULAVIO na MARULLO	Mawakili
ARITEMIDORO	Mwalimu wa ufasaha
Mtabiri	
SINNA	Mshairi
Mshairi mwingine	
LUSILIO, TITINIO MESSALA, KATO kijana, VOLUMNIO	Marafiki wa Buruto na Kasio
VARRO, KILITO KILAUDIO, STIRATO LUKIO, DARIDANIO	Watumishi wa Buruto
PINDARO	Mtumishi wa Kasio
KAPUNIA	Mke wa Kaizari
POSHIA	Mke wa Buruto

Maseneta, Raia, Walinzi, Wafuasi, n.k.

MAONYESHO: Kwa sehemu kubwa ya mchezo, mjini Roma; baadaye Sardisi, na ujirani wa Filippi.

I

Onyesho la I: Roma. Barabarani

(*Wanaingia Fulavio, Marullo na raia wengine*)

FULAVIO: Haya! Makwenu, nyie viumbe wazembe, makwenu!
Je, hii ni siku kuu? Hamjui kuwa ninyi
Wote ni vibarua tu, hivyo hamna ruhusa
Kutoka na kutembea siku iliyo ya kazi
Bila kuwa na alama ya kazi mzifanyazo?
Wewe, kazi yako nini?

RAIA 1: Mimi, bwana, seremala.

MARULLO: I wapi nguo yako ya kazi na chenezo yako?
Kwa nini leo umevaa nguo zako rasmi?
Wewe, bwana, kazi yako?

RAIA 2: Kwa kweli, bwana, kwa kufuata mfanya kazi bora,
Mimi, waweza kusema, ni mlea viatu tu.

MARULLO: Nijibu waziwazi, wewe kazi yako ni nini?

RAIA 2: Kazi, bwana, ambayo natumaini naweza kuifanya
Kwa moyo safi; mimi kwa kweli ni mganga wa nyayo
Mbovu.

MARULLO: Kazi gani, fidhuli wee? Unafanya kazi gani?

RAIA 2: La, nakusihi, bwana, usinipayukie; lakini ikiwa
Utanipayukia, naweza nikakuponya.

MARULLO: Maana yake nini? Uniponye, fidhuli wee!

RAIA 2: Naam, bwana, kukutia wayo.

FULAVIO: U fundi viatu, siyo?

RAIA 2: Kwa kweli, bwana, nipatiacho riziki yangu ni
Msharasi: sijiingizi katika mambo ya wafanya kazi wala
Ya wanawake; lakini hata hivyo, bwana, mimi ni mganga
Wa viatu vikuukuu; vinapokuwa hatarini naviponya.

Watu wote wa maana ambao wamepata kukanyaga
Ngozi wametembea juu ya kazi yangu.

FULAVIO: Lakini kwa nini leo huko kwako kiwandani?
Kwa nini wawatembeza hawa mabarabarani?

RAIA 2: Kwa kweli, bwana, kuchakaza viatu vyao, ili
Nijipatie kazi zaidi. Mzaha mbali, bwana,
Tumejipa sikukuu ili tumwone Kaizari na kufurahia
Shangwe yake.

MARULLO: Mnafurahia nini? Analeta nyara gani?
Mateka gani wafungwa wamfuatia Roma;
Ili kustahilisha mapito ya gari lake?
Enyi magogo, enyi mawe, enyi anzali duni
Kuvizidi viumbe visivyokuwa na akili!
Enyi mioyo migumu, O, makatili wa Roma,
Hamkumjua Pompe? Mara ngapi mmepanda
Vyambazani, burujini, minara na madirisha,
Naam, hata juu ya mabomba ya majikoni,
Na vyana vyenu vichanga mkibeba mikononi,
Nako mkashinda kutwa, kwa saburi na shauku,
Kumwona Pompe mkuu ata'popita katika
Mabarabara ya Roma:
Na mara mlipoona gari lake kutokea,
Hamkumshangilia kwa sauti ilofanya
Hata mto Tiberia utikisike kingoni,
Kwa kule kuusikia mwangwi wa sauti zenu
Uliofanywa katika uvungu wa pwani zake?
Je, na sasa mwavalia nguo zenu malidadi,
Je, na sasa mnajipa siku ya kuacha kazi,
Je, na sasa mwatapanya maua kwenye mapito
Ya ajaye akitamba kwa kuua wana Pompe?
Ondokeni!
Kimbilieni makwenu, mwende mpige magoti
Na kuiomba miungu iliahirishe janga
Litaloletwa na huu utovu wa shukurani.

FULAVIO: Nendeni, wananchi wema, na kwa kosa
Lenu hili,
Nendeni mkakusanye fukara wenzenu wote;
Wapelekeni kingoni mwa mto wa Tiberia,
Mkalilie machozi yenu mwenye mto huo,
Hata mto ufurike kwenye kingoze za juu.

(*Raia wanaondoka*)

Tazama, hapana mwovu kati yao asopatwa!
Wametoka kwa fadhaa, sababu ya kosa lao.
Wewe nenda pita huku kwelekea Barazani.
Mimi nitapita huku. Sanamu zivue nguo,
Ikiwa utazikuta zimepambwa kwa sherehe.

MARULLO: Twaweza kufanya hivyo? Hujui ya kuwa leo,
Inaadhimishwa siku kuu ya Luparekali?

FULAVIO: Haidhuru; zisibaki sanamu zilizovishwa
Hidaya za Kaizari. Mimi nitapita huku
Na kuwafukuza kina yahe mabarabarani.
Na wewe kafanye vivyo ukiwakuta po pote
Walipofanya makundi. Manyoya haya yaliyo
Mbawani mwa Kaizari kama yakinyonyolewa,
Atawezeshwa kuruka urefu wa kawaida.
Ambaye pasipo hivyo atapanda watu juu
Na sote akatuweka kwenye hofu ya kitumwa.

(*Wanatoka*)

Onyesho la II: Hadharani

(*Wanaingia wakiandamana kwa muziki, Kaizari, Antonio, Kapunia, Poshia, Desio, Sisero, Buruto, Kasio, na Kasika; na kundi kubwa likifuatana; na Mpiga Ramli miongoni mwao*)

KAIZARI: Kapunia!

KASIKA: Kimya, kimya, nyamazeni!

(*Muziki unanyamaa*)

KAIZARI: Kapunia!

KAPUNIA: Labeka, Seyyid yangu.

KAIZARI: Simama katika njia ya Mariko Antonio
Akimbiapo katika mapito yake. Antoni!
ANTONIO: Kaizari, bwana wangu!
KAIZARI: Utapokuwa mbioni, Antonio, ukumbuke
Kumgusa Kapunia, maana wazee wetu
Husema kuwa katika mbio hizi takatifu
Wanapoguswa wagumba, ugumba wao hutoka.
ANTONIO: N'takumbuka:
Kaizari akisema 'fanya hivi', hufanyika.
KAIZARI: Haya, anza; na usisahau tambiko lo lote.

(*Muziki*)

MPIGA RAMLI: Kaizari!
KAIZARI: Ho! nani anayeita?
KASIKA: Ambia kila kelele inyamaze:—kimya tena!

(*Muziki unanyamaa*)

KAIZARI: Ni nani humu kundini ambaye ananiita?
Ambaye ana ulimi unaozidi muziki,
Ukiita 'Kaizari'. Sema, anasikiliza.
MPIGA RAMLI: Jihadhari na tarehe ya katikati ya Machi.
KAIZARI: Mtu gani huyo?
BURUTO: Ni mganga wa ramli ambaye anakuomba
Utahadhari tarehe ya katikati ya Machi.
KAIZARI: Mleteni mbele yangu: niuone uso wake.
KASIO: Wewe, ondoka kundini, ukamwone Kaizari.
KAIZARI: Una habari gani za kun'ambia? Sema tena.
MPIGA RAMLI: Jihadhari na tarehe ya katikati ya Machi.
KAIZARI: Huyu ni muota ndoto; tumwache: haya piteni.

(*Muziki. Wote wanaondoka ila Buruto na Kasio*)

KASIO: Utakwenda kutazama njia watakayopita?
BURUTO: Siyo mimi.
KASIO: Nakusihi sana, nenda.
BURUTO: Mimi sipendi michezo: moyo wangu haunayo
Hali ya kutaanasa alo' nayo Antonio.
Usinijali, Kasio, timiza mapenzi yako.

Mimi nitakwenda zangu.
KASIO: Buruto, nimekuwa nakuchungua siku hizi:
Sioni machoni mwako hali ile ya upole,
Na dalili ya mapenzi ulivyokuwa zamani:
Tabiayo imekuwa ni ya ubaridi mno,
Tena ya kigeni sana kwa rafikiyo mpenzi.
URUTO: Kasio, 'sidanganyike; kama najificha uso,
Taabu za moyo wangu najirudishia kwangu.
Kweli ninasumbuliwa siku hizi na mawazo
Ambayo yanapingana, yanihusuyo mwenyewe,
Labda ndiyo yatiayo dosari tabia yangu;
Bali marafiki zangu hiyo isiwahuzunishe—
Nao miongini mwao, Kasio, u mmojapo—
Wala wasilipe kosa langu maana zaidi,
Ila kwamba maskini Buruto apiganapo
Na nafsiye mwenyewe husahau kuonyesha
Dalili zenye mapenzi kwa binadamu wengine.
KASIO: Kwa hiyo, Buruto mwema sikukuelewa vema:
Na kwa hiyo nimeficha humu kifuani mwangu
Mawazo ya tunu kuu yanayotaka fikara.
Nambie, Buruto mwema, unaweza kujiona?
BURUTO: La, Kasio, kwani jicho haliwezi kujiona
Ila tu kwenye mfano katika vitu vingine.
KASIO: Sawa; na yasikitisha sana Buruto ya kuwa
Wewe hunavyo vioo kama hivyo vya kuweza
Kukwonyesha utukufu wako uliofichika,
Ili mwenyewe uweze kuiona sura yako.
Nimewasikia wengi watu azizi wa Roma—
Kumwondoa Kaizari wa milele— wakisema,
Wamtajapo Buruto huku wakilalamika
Chini ya utumwa huu uwaumizao sasa,
Wangependa mtukufu Buruto awe na macho.
BURUTO: Wapenda kuniingiza katika hatari gani,
Kasio, kwa kunitaka nitafute nafsini

Kile ambacho sinacho katika nafsi yangu?
KASIO: Kwa hiyo, Buruto mwema, kuwa radhi usikie.
Na kwa sababu wajua huwezi ukajiona
Mimi, ni kioo chako, nitakwonyesha kidogo
Kile kitu juu yako ambacho hujakijua.
Na wala Buruto mwema, sinitilie mashaka:
Ningekuwa mdhihaki, nalifuja pendo langu
Kwa kumpa urafiki kila mjipendekeza;
Au kama wanijua, kuwa huwarai watu,
Na nikawabusu sana, kisha nikawakashifu;
Au najipendekeza, nakirimu kina yahe,
Basi, hapo unifanye kuwa ni mtu hatari.
(*Shangwe na kelele*)
BURUTO: Kelele hizo za nini? Isije ikawa watu
Wamfanya Kaizari kuwa mfalme wao.
KASIO: Isije ikawa? Basi n'seme hungependa iwe?
BURUTO: Nisingependa, Kasio, bali nampenda sana.
Walakini ni kwa nini wanicheleweshа hivi?
Ni jambo gani ambalo ungependa kunambia?
Kama ni jambo ambalo lina faida kwa umma
Weka utu jicho moja, na kifo jicho la pili,
Nitaviona ni sawa; kwani miungu shahidi,
Napenda utu kuzidi ninavyokihofu kifo.
KASIO: Najua sana, Buruto, unacho kipawa hicho,
Kama ninavyoyajua maungo na sura yako.
Basi, utu ndiyo kisa cha mazungumzo yangu.
Siwezi kukuambia wewe na watu wengine
Mnafikiria nini juu ya maisha haya:
Bali kwa upande wangu ni heri nisiwe hai
Kuliko nikiwa hai na kukiogopa kitu
Ambacho ni chenye hali iliyo sawa na yangu.
Mimi nilizawa huru, kama yeye Kaizari;
Na wewe ni kadhalika. Sote tumekula sawa,
Na twaweza kuhimili baridi kali kamaye.

Kwa sababu siku moja yenye baridi ajabu,
Na mto wa Tiberia umejaa hadi juu,
Na tena umechafuka, Kaizari alisema,
'Unathubutu Kasio, kujitosa nami sasa,
Mwenye jito kali hili, twogelee hadi kule?'
Pale pale na mavazi yale yale n'kajitosa
Na kumwomba afuate: na kweli akafuata.
Dhoruba ikanguruma, na sisi tukaichapa
Kwa mikono mishupavu tukiitupa pembeni
Na kuipiga vifua kwa nyoyo za ushindani.
Lakini tungali bado kupakaribia pale
Pahali palipotajwa, Kaizari alilia,
'Nisaidie, Kasio, au sivyo nitazama!'
Mimi, kama Aenea, babu yetu maarufu,
Alivyobeba begani mzee Anikisesi,
Na kumwokoa kutoka kwenye mto wa Troyi,
Ndivyo nilivyomwokoa taabani Kaizari
Kutoka kwenye mawimbi ya mto wa Tiberia.
Naye mtu huyu sasa amekuwa ni muungu,
Na Kasio ni kijitu duni ambacho lazima
Kisujudu Kaizari japo kakiona tu.
Alikuwa ana homa kule Hispaniola.
Nayo ilipomzidi nilimwona kutetema:
Naam, muungu huyu, ni kweli alitetema:
Midomo yake mioga ikawa haina rangi.
Na jichole lile lile litishalo ulimwengu
Lilitokwa nuru yake. Nilisikia alia,
Naam na ulimi wake uloamuru Warumi
Wamsikilize vema, waandike hotubaze
Katika vitabu vyao, ole wake! ulilia,
'Nipe kinywaji, Titinio!' kama mwali mgonjwa.
Enyi miungu nashangazwa mtu dhaifu hivyo
Anaweza kuongoza dunia tukufu hii
Na kufaidi pekee.

(*Shangwe na kelele*)

BURUTO: Kelele nyingine tena! Naamini shangwe hizo
Ni shangwe za vyeo vipya apewavyo Kaizari.
KASIO: Sawa, kwani atagaa dunia nyembamba hii
Kama jitu, na vijitu kina sisi tunapita
Chini ya miguu yake na kuchungulia kote
Na kujikuta katika makaburi ya fedheha.
Watu wakati mwingine hutawala sudi zao:
Kosa, mpenzi Buruto, si kosa la nyota zetu,
Kwamba tu watu wa chini, bali ni letu wenyewe.
Buruto na Kaizari: 'Kaizari' lina nini
Hata litajwe zaidi kulipita jina lako?
Yaandike kwa pamoja, lako zuri kama lake;
Yatamke ulimini, yote yanaupendeza;
Yapime kwenye mizani, lako zito kama lake;
'Kiyapungia shetani, 'Buruto' lina uweza
Wa kumleta haraka kama hilo 'Kaizari.'
Basi, kwa majina ya miungu yote kwa pamoja,
Huyu Kaizari wetu chakula chake ni nini,
Hata akavimba hivyo? Rika, umefedheheka!
Roma, ume'sha poteza vizazi vya watu bora!
Tangu lini kumekuwa, tokea gharika kuu,
Wakati ul'otukuka kwa sifa ya mtu mmoja?
Ni lini, kuacha sasa, wangeweza wakasema,
Waliokitaja Roma, kwamba kuta zake pana
Zina mtu mmoja tu? Sasa ndiyo Roma kweli
Ambayo ina nafasi ya mtu mmoja, basi.
O! wewe na mimi pia tumepata kusikia
Wazee wetu kusema, alikuwapo Buruto
Ambaye kumkubali mfalme hapa Roma
Ni sawa na kukubali Shetani akatawala.
BURUTO: Ya kwamba unanipenda sina shaka asilani;
Unalonishawishia naweza kubahatisha;
Nilivyolifikiria pamwe na nyakati hizi,

Nitakweleza halafu: kwa sasa ninakusihi
Kwa mapenzi, sitaweza kushawishika zaidi:
Uliyokwisha kusema, mimi nitayafikiri;
Nayo utakayosema, nitasikiliza vema,
Na kutafuta wakati ufaao kusikia,
Na kujibu kwa saburi majambo makubwa hivyo.
Na mpaka wakati huo, rafiki yangu mwadhamu,
Kaa ukiwaza haya: ni heri Buruto awe
Mshamba wa kijijini, kuliko kujitukuza
Kuwa ni mwana wa Roma, kwenye hali mbaya hii
Iwezayo ikaletwa kwetu na nyakati hizi.

KASIO: Nafurahi kuwa haya maneno yangu dhaifu
Yameweza yakawasha angao cheche la ari
Kutoka kwake Buruto.

BURUTO: Michezo imekwisha na Kaizari anarudi.

KASIO: Watapopita mvute Kasika kwa nguo yake
Naye atakuambia, kwa jinsiye kisirani,
Jambo lo lote la ma'na lililotokea leo.

(*Aingia tena Kaizari na wafuasi wake*)

BURUTO: Vyema, nitafanya hivyo. Bali, tazama, Kasio,
Kaizari aoneka kuwa amekasirika,
Na wengine wote kama kwamba wamekaripiwa:
Uso wake Kapunia umefifiwa na rangi;
Na Sisero macho yake yamegeuka mekundu
Kama vile tumwonavyo awapo kakasirishwa
Na maseneta fulani katika Baraza Kuu.

KASIO: Kasika atakwambia nini kilichotokea.

KAIZARI: Antonio!

ANTONIO: Kaizari!

KAIZARI: Napenda karibu yangu watu walio wanene;
Wenye vichwa viororo na walalao fofofo;
Yule Kasio ni mwenye uso njaa na mwembamba;
Afikiri mno: watu wa jinsiye ni hatari.

ANTONIO: Simwogope, Kaizari ye si mtu wa hatari;

Ni Mrumi mtukufu tena mwenye nia safi.
KAIZARI: Bor'angekuwa mnene! Walakini simwogopi:
Ila kama jina langu lingeogopa cho chote,
Sijui ni mtu gani ningemwambaa mapema
Kama ningemwambaavyo Kasio mwembaba yule.
Ni mchunguzi mkuu, na huyaona kwa ndani
Matendo ya binadamu; wala hapendi michezo,
Kama wewe, Antonio; hasikilizi muziki:
Hacheki ila kwa shida, na hapo anapocheka,
Huwa kama asimanga na kubeza moyo wake
Kwa kuwa umekubali kuchekeshwa na cho chote.
Watu kama jinsi yake hawana raha moyoni
Wanapomwona mwingine mkubwa wa kuwazidi,
Na kwa hiyo watu hao ni watu hatari sana.
Nakuambia ni nini kifaacho kuogopwa,
Siyo nikiogopacho; kwani ndimi Kaizari.
Nj'o huku kulia kwangu, sikio hili si zima,
Unambie kwa yakini unavyomfikiria.

(*Wanatoka isipokuwa Kasika. Mlio wa tarumbeta. Kaizari na watu wote*)

KASIKA: Ulinivuta kwa joho; wataka kusema nami?
BURUTO: Ndiyo, Kasika; twambie yaliyotokea leo,
Kumfanya Kaizari awe amenuna hivyo.
KASIKA: Ala! Ulikuwa pamoja naye, siyo?
BURUTO: Basi 'singekuuliza yal'otokea, Kasika.
KASIKA: Aa! Alipewa taji, na baada ya kupewa, akalikataa hivi, kwa mkono wake; na hapo watu wakaanza kupiga kelele.
BURUTO: Ile kelele ya pili ilikuwa ni ya nini?
KASIKA: Kwa sababu hiyo hiyo.
KASIO: Walipiga mara tatu; kelele ya tatu nayo
Ilikuwa ni ya nini?
KASIKA: Kwa sababu hiyo hiyo.
BURUTO: Je, wasema alipewa hilo taji mara tatu?

KASIKA: Naam, na akalikataa mara tatu, lakini kwa
shingo upande zaidi kuliko kwanza, na kila
alipolikataa, majirani zangu akina yahe wakapiga
makelele.
KASIO: Nani alimpa taji?
KASIKA: Antonio.
BURUTO: Twambie ilivyokuwa, Kasika mpole sana.
KASIKA: Nawezaje kuwaambieni ilivyokuwa?
Ulikuwa unafiki mtupu; sikuujali. Nilimwona
Mariko Antonio akimpa taji – wala halikuwa taji,
ulikuwa ni mfano wa kitaji tu; na kama nilivyosema
alilikataa mara ya kwanza; lakini kwa kweli
nilivyofikiri alisebusebu. Halafu akampa tena,
naye akalikataa tena; lakini nilivyofikiri
hakupenda hata kidogo kuliachia.
Halafu akampa mara ya tatu; akaliweka chini tena
mara ya tatu: na kila alipolikataa akina yahe
walipiga kelele na kupiga makofi na kuzitupa
hewani kofia zao zilizokuwa zimelowa kwa majasho
na kutoa harufu mbaya sana, ati kwa sababu
Kaizari alikuwa amekataa taji, hata ilikuwa
karibu kumsonga roho Kaizari mwenyewe; kwani
alizimia na kuanguka: na nafsi yangu sikuthubutu
kucheka kwani nilihofu kupanua kinywa changu
na kupokea harufu chafu.
KASIO: Lakini, wasemaje: Kaizari alianguka?
KASIKA: Alianguka hadharani, na kutoka povu kinywani
na hakuweza kusema.
BURUTO: Inawezekana sana; maana ana kifafa.
KASIO: La, yeye hana kifafa: ila ni wewe, na mimi,
Na Kasika mwaminifu, ni sisiwenye kifafa.
KASIKA: Sijui maana yako ni nini kwa kusema hivyo:
lakini nina hakika Kaizari alianguka. Ikiwa
kina yahe hawakumshangilia na kumpepea kufuata

jinsi alivyowapendeza na kuwachukiza, namna wawafanyiavyo wachezaji katika nyumba za michezo, basi mimi ni mwongo.

BURUTO: Na alipozindukana alisema kitu gani?

KASIKA: Lo, kabla hajaanguka, alipoona kuwa kina yahe walifurahi kwa kuwa alikataa taji alifungua ukosi wa koti lake, na kuwapa koo lake walikate; na kama ningalikuwa mtu wa hivi hivi ningalimkubalia, nikawa shetani miongoni mwa wahuni. Basi, akaanguka. Alipozindukana akasema kuwa ikiwa alitenda au kusema jambo lo lote lisilostahili, aliwaomba watukufu hao wajue kuwa ilikuwa ni udhaifu wake. Hayawani watatu au wanne, karibu na pahali nilipokuwa nimesimama, wakamsikitikia, 'Masikini wee!', na kumsamehe kwa mioyo yao yote; lakini hapana haja kuwajali: kama Kaizari angekuwa amewachinja mama zao, wasingetenda lo lote zaidi.

BURUTO: Na ba'da ya hayo akaondoka kanuna hivyo?

KASIKA: Naam.

KASIO: Je, Sisero alisema cho chote?

KASIKA: Naam, alisema Kigiriki.

KASIO: Alisema nini?

KASIKA: Lo, nikiweza kukuambia sintaweza tena kukutazama usoni. Lakini waliomwelewa walichekeana na kutikisa vichwa; ila kwangu mimi kilikuwa ni Kigiriki kitupu. Ningeweza kuwaambieni habari zaidi: Marullo na Fulavio, kwa kuzivua nguo sanamu za Kaizari, wameuzuliwa. Kwa herini. Kulikuwa na upumbavu mwingi zaidi kama ningeweza kuukumbuka.

KASIO: Waweza kula na mimi leo usiku, Kasika?

KASIKA: La, nimeahidi kwingine.

KASIO: Utakula nami kesho?

KASIKA: Naam, nikiwa hai, na wewe usipobadili nia, na
chakula chako kikiwa kinalika.
KASIO: Vyema; n'takutazamia.
KASIKA: Nitazamie: kwa herini nyote.

(*Kasika anatoka*)

BURUTO: Mbona kawa ovyo hivi: alipokuwa shuleni
Alikuwa chapu chapu.
KASIO: Bado hajabadilika, yungali ni yule yule,
Katika kutekeleza lo lote la ushujaa,
Au la utu, ingawa aonekana mzembe.
Ufidhuli wake huu ni kama kitoweo tu,
Kiwapacho wanadamu matumbo ya kuyeyusha
Maneno yake machungu.
BURUTO: Bila shaka hivyo ndivyo. Kwa sasa nitakuacha:
Kesho kama utapenda kuzungumza na mimi,
Nitaweza kuja kwako; au kama ukipenda,
Utaweza kuja kwangu, nami nitakusubiri.
KASIO: Nitafanya hivyo. Mpaka hapo waza ya dunia.

(*Buruto anatoka*)

Kweli, Buruto u mtu mwema, lakini naona
Tabia yako tukufu yaweza ikageuzwa
Iache asili yake. Ndiyo maana ni bora
Watu watukufu wawe daima na wenzi wao;
Kwani nani ni imara hata asishawishike?
Kaizari hanipendi; anampenda Buruto:
Ningelikuwa Buruto, naye awe ni Kasio,
Kamwe asingeniweza. Usiku huu wa leo,
Nitatupa dirishani kwake hati mbalimbali,
Kama kwamba zimetoka kwa raia mbalimbali,
Na zitataja sifaze katika mji wa Roma.
Na Kaizari kupenda cheo n'tataja kwa hila
Basi baada ya hapo Kaizari ahadhari,
Kwani tutamtikisa, ama tustahimili
Taabu nyingi zaidi.

(*Anatoka*)

Onyesho la III: Barabarani

(*Ngurumo na umeme. Wanaingia, kutoka pande zote mbili, Kasika, kachomoa upanga wake, na Sisero*)

SISERO: Masalkheri, Kasika! Je, ulimsindikiza
Kaizari kwake? Mbona wahema, watoa macho?
KASIKA: Wewe wala hustuki, ambapo dunia nzima,
Inayumbayumba hivi, mithili kitu dhaifu?
O Sisero, nimepata kushuhudia dhoruba,
Pepo kali zikaweza kuvunja hata mibuyu;
Nimeiona bahari ikivimba na kufura,
Kwa mawimbi na mapovu, kama kwamba inataka
Kuyafikia mawingu: bali dhoruba ya moto,
Sijapita asilani, ila usiku wa leo,
Ila sasa hivi tu. Au kuna vita juu,
La sivyo, dunia hii imeiudhi miungu,
Kiasi cha kuifanya ilete maangamizo.
SISERO: Vipi, umeona jambo linaloshangaza sana?
KASIKA: Mtumwa wa kawaida – wamjua ukimwona –
Aliinua mkono wake wa kushoto nao
Ukawaka na kung'aa kama myenge ishirini,
Na wala usiungue.
Pia – sijaurudisha upanga wangu alani –
Nilikutana na simba karibu na Barazani,
Aliyenikodolea na kwenda kakasirika,
Wala bila kunidhuru: wanawake mia moja
Walosongana kwa hofu hata sura kugeuka;
Waliapa wameona watu wawakao moto
Wakitembeatembea huko mabarabarani.
Tena jana alasiri bundi katua sokoni
Na kulia kwa kelele. Maajabu kama haya,
Yanapokuja pamoja, si vema watu kusema:
Sababu zake ni hizi; ni mambo ya kawaida,
Kwani mimi naamini ni ishara za majambo
Ambayo zayabashiri.

SISERO: Kweli, huu ni wakati wa majambo ya ajabu.
Ila watu wanaweza kubashiri matukio
Vile wapendavyo wao, namna mbali kabisa
Na makusudio hasa ya matukio yenyewe.
Je, kwa kesho Kaizari atakuja Barazani?
KASIKA: Atakuja: kwa sababu alimtuma Antoni
Akufahamishe kuwa atakuwapo kwa kesho.
SISERO: Basi, kwa heri, Kasika: wingu hili chafu mno;
Siyo la kutembelea.
KASIKA: Haya, kwa heri Sisero.

(*Sisero anatoka*)

(*Kasio anaingia*)

KASIO: Nani huyo?
KASIKA: Mrumi.
KASIO: Ni Kasika kwa sauti.
KASIKA: Wasikia vema. Kasio, usiku gani huu?
KASIO: Usiku mzuri sana kwa watu waaminifu.
KASIKA: Nani kapata kuona mbingu ikitisha hivi?
KASIO: Wanaojua dunia na machafu yake mengi.
Nimetembeatembea mimi mabarabarani
Nikijitosa katika usiku hatari huu,
Na kama unionavyo, Kasika, na bila nguo,
Nimejiweka kifua wazi dhorubani humu;
Na umeme samawati ulipojipindapinda
Kama unaopasua kifua cha mbingu, mimi
Nilijitia kabisa ndani ya shabaha yake.
KASIKA: Lakini kwa nini hasa kuchokoza mbingu hivyo?
Yawapasa binadamu kuhofu na kutetema,
Miungu yenye uwezo iletapo kwa ishara
Ujumbe wa kuogofya hivi ili kututisha.
KASIO: Umepooza, Kasika; nazo cheche za maisha
Ambazo kila Mrumi yampasa kuwa nazo,
Huna au hutumii; umefifiliwa rangi,
Macho umeyakodoa, na umejivisha hofu

Na shangao kwa kuona vioja hivi vya mbingu:
Lakini ungefikiri sababu ya kweli hasa,
Kwa nini mioto hii na pepo wanyinyirika,
Kwa nini ndege na nyama kuacha tabia yao—
Wazee kuwa wajinga, watoto kuwa werevu,
Vipi vitu vyote hivi vyabadili hali yao
Ya kanuni na asili vikawa ni madubwana;
Bila shaka utaona mbingu imevifukiza
Hali hii kuvifanya vyombo vya kuleta hofu
Na maonyo kwa sababu ya hali fulani mbaya.
Ningeliweza, Kasika, kukutajiaye mtu,
Ambaye ni sawasawa na usiku mbaya huu,
Ambaye huunguruma, humulika kama radi,
Hufungua makaburi, na kuvuma kama simba
Avumavyo Barazani, – mtu asiyekuzidi
Wala asiyenizidi kwa kitendo chake yeye,
Lakini ambaye kawa mkubwa na wa kutisha
Sawa na msukosuko wa ajabu kama huu.

KASIKA: Wasema Kaizari, ama si yeye, Kasio?

KASIO: Haidhuru awe nani, kwani Warumi wa leo
Wana nguvu na viungo sawa na vya babu zao;
Ila, ole wetu! vichwa vya mababu vimekufa,
Nasi tunatawaliwa na roho za mama zetu;
Utumwa na ta'bu zetu hizi zinathibitisha
Kuwa sisi sote sasa tumekuwa wanawake.

KASIKA: Kwa kweli yasemekana ya kuwa kesho wajumbe
Wanataka kumfanya Kaizari mfalme;
Na tajile atavaa baharini na barani,
Mahali po pote pale ila hapa Italia.

KASIO: Hapo nitajua wapi kutumia singe hii;
Kasio tamkomboa Kasio toka ujani.
Hapo enyi, e miungu, ndipo mnapomfanya
Mnyonge kuwa na nguvu; hapo enyi, e miungu,
Ndipo mnapowashinda wale walio dhalimu.

Hapana ngome ya mawe, kuta za shaba thabiti,
Gereza iso na hewa, au ni pingu za chuma,
Ambazo zina uwezo kufunga nguvu za moyo.
Bali uhai ukisha kuchoshwa na pingu hizi
Za dunia haukoswi nguvu za kujimaliza.
Mimi nikijua hivyo, pia dunia yajua,
Chembe ile ya dhuluma ambayo ninaibeba
Naweza nikajivua kadiri ninavyopenda.

(*Bado ngurumo*)

KASIKA: Na mimi pia naweza. Na kwa njia hiyo hiyo
Kila mtumwa anao, katika mikono yake,
Uwezo wa kumaliza utumwa wake mwenyewe.

KASIO: Na kwa nini Kaizari awe mdhalimu, sasa?
Maskini! Natambua hangekuwa mbwa mwitu
Ila kwa kuona kuwa Warumi ni kondoo tu:
Yeye hangekuwa simba Warumi wasingekuwa
Ni makoo ya paa tu.
Wenye haraka ya moto huuanza kwa vijani:
Roma umekuwa taka, umekuwa ni jalala,
Umekuwa upuuzi, kutumiwa kama nyasi
Za kumulikia kitu duni kama Kaizari.
Ole wangu, a, huzuni, umenifikisha wapi?
Pengine nasema haya na mtu mpenda uja:
Kama ndivyo, jibu langu lazima liwe tayari;
Bali ninayo silaha, na hatari sizijali.

KASIKA: Unasema na Kasika; na mtu ambaye kamwe
Hana udhabidhabina. Ushike mkono wangu:
Kajiundieni njama kutoa maovu haya;
Na huu mguu wangu nitaufikisha kote
Utakakofika wake mtangulizi kabisa.

KASIO: Basi tumepatana. Sasa fahamu, Kasika,
Nimeshawishi tayari, Warumi fulani bora,
Kushirikiana nami ili kutenda kitendo
Cha heshima na hatari. Najua, kwa njia hii,

Ya kwamba kwa hivi sasa wako wananisubiri
Kwenye ukumbi wa Pompe. Kwani usiku watisha
Na hakuna majiani ghasia na kutembea.
Na hali hii ni sawa na kazi tuitakayo,
Ya damu, na kali sana, yenye kutisha kabisa.

KASIKA: Jifiche kwanza, naona aja mtu kwa haraka.

KASIO: Ni Sinna; – namjua kwa mwendo wake; ni rafiki.

(*Aingia Sinna*)

Sinna, mbona una hima, una hima kwenda wapi?

SINNA: Kukutafuta. Huyo ni nani, Mettello Simberi?

KASIO: Hasha, siye, ni Kasika; naye ni mmoja wetu
Katika shughuli zetu. Nangojewa huko, Sinna?

SINNA: Nafurahi. Usiku gani huu! Wawili wetu
Au watatu wameyaona mambo ya ajabu.

KASIO: Nangojewa? Niambie.

SINNA: Naam, unangojewa. A, Kasio, ungeweza
Kumpata mtukufu Buruto upande wetu—

KASIO: Kuwa radhi: Sinna mwema, twaa karatasi hii,
Ukaiweke vizuri chini ya kikao chake,
Ambapo ni Buruto tu awezaye kuiona;
Na hii kamtupie katika dirisha lake;
Hii kaibandikize kwa nta kwenye sanamu
Yake Mzee Buruto; ukisha timiza hayo,
Rudi – na utatukuta kwenye ukumbi wa Pompe.
Desio Buruto na Tirebonio wako huko?

SINNA: Wote wako, kuondoa Metello Simberi peke,
Ambaye kenda nyumbani kwako kukutafutawe.
Nitakwenda hima hima, ili nikazitapanye
Karatasi hizi kama ulivyoniagizia.

KASIO: Ukimaliza, rejea kwenye ukumbi wa Pompe.

(*Sinna anaondoka*)

Njoo, Kasika, kabla ya kesho wewe na mimi
Twaweza kwenda kumwona Buruto nyumbani kwake:
Robo tatu zake sasa zime'sha kuwa ni zetu,

Na tukutanapo tena atajitolea kwetu.
KASIKA: A, anapendwa katika mioyo ya watu wote:
Na kile ambacho kwetu kingekuwa ni hatia
Kukubali kwake yeye kutakuwa ni uganga
Na kukifanya kikawa ni wema na ustahiki.
KASIO: Umetambua vizuri, jinsi tumhitajivyo,
Nao utukufu wake. Haya basi twende zetu.
Kwani sasa ni zaidi ya saa sita usiku,
Na kabla hakujacha tutakwenda tumwamshe
Tuwe na hakika naye.

(*Wanatoka*)

II

Onyesho la I: Roma. Katika Bustani ya Buruto

(*Aingia Buruto*)

BURUTO: Nini, Lukio, he?
Kwa kuangalia nyota siwezi nikakisia
Kama ku karibu kucha.
Lukio, nakuita! – Na mimi ningefurahia
Kosa la kulala sana hivyo. - Sa'ngapi, Lukio?
Saa ngapi? Wee, amka! Kuna nini, Lukio!

(*Lukio anaingia*)

LUKIO: Uliniita, bwanangu?
BURUTO: Kapeleke mshumaa chumbani kwangu, Lukio,
Na ukisha kuuwasha rudi uje uniite.
LUKIO: Ee walla, bwana wangu.

(*Anatoka*)

BURUTO: Hana budi auawe: japo kwa upande wangu
Sinayo sababu yangu, kufanya nimchukie,
Ila sababu ya umma: ataka avikwe taji –
Jambo hilo linaweza kubadili hali yake.
Ni siku ya jua kali nyoka atokapo nje,
Na inofaa hadhari. Mvike taji kichwani?
Basi hapo sina shaka tutamtilia sumu
Ambayo itamwezesha kuwa mwovu apendavyo.
Kukufuru kwa ukubwa ni pale unapotenga
Huruma na mamlaka: na kwa kweli sikumbuki
Muda wo wote ambapo mapenzi ya Kaizari
Yameshinda akilize. Lakini ni wazi kwamba
Unyenyekevu ni ngazi ya kila mtaka cheo,
Ambayo anayepanda huitazama kwa juu,

Bali akisha kanyaga kile kipago cha mwisho
Mara huipa kisogo ngazi aliyopandia,
Akatazama mawingu na kudharau vya chini.
Kaizari anaweza. Ili asiweze, kinga.
Na kwa kuwa kisa hiki hakifanani alivyo
Ni bora kizushwe hivi: ya kwamba hivi alivyo
Kama akiongezewa hana budi atavuka
Mipaka kadha wa kadha; na kwa hivyo mfikiri
Sawa na yai la nyoka; kama akitotolewa,
Tafuata ada yao na kuyatenda maovu;
Basi mwulie gandani.

(*Lukio anarudi*)

LUKIO: Mshumaa unawaka chumbani mwako, hababi.
Niliponikitafuta kijiti kwa dirishani
Nilikuta karatasi inao muhuri hivyo:
Najua haikuwapo nilipokwenda kulala.

(*Anampa barua*)

BURUTO: Rudi ukalale tena. Usiku bado mkubwa.
Ati, kesho ni tarehe ya katikati ya Machi?
LUKIO: Sifahamu, bwana wangu.
BURUTO: Kaitazame kalenda, uniletee habari.
LUKIO: Ee walla, bwana wangu.

(*Lukio anatoka*)

BURUTO: Vimwondo hivi hewani jinsi vipitapitavyo,
Vina nuru ya kutosha kuniwezesha kusoma.

(*Anafungua barua na kusoma*)

'Buruto umelala: amka ili ujione.
Je, Roma, n.k. Tamka, anza, lete uokovu.
Buruto umelala: amka!' Chonjo kama hizi
Mara nyingi zimepata kudondoshwa na kuachwa
Mahali ambapo baadaye nimeziokota.
'Je, Roma, n.k.' Sina budi nitafsiri hivi:
'Roma, izidi kumwogopa mtu mmoja?' Roma?
Lo, wazee wangu walimfukuza Tarikwini

Katika njia za Roma alipoitwa mfalme.
'Tamka, anza, lete uokovu!' Wananisihi
Nitamke, na nianze? O, Roma, nakuahidi,
Kama wokovu ukija utakuwa umepata
Ombi lako kamilifu kwa mkono wa Buruto.

(*Lukio anarudi tena*)

LUKIO: Bwana, Machi sasa unazo siku kumi na tano.

(*Hodi kwa ndani*)

BURUTO: Vema, nenda mlangoni: kuna mtu anabisha.

(*Lukio anatoka*)

Tangia siku Kasio aliponiwasha moyo
Kuchukia Kaizari sijapata usingizi.
Kati ya kutenda baya na tangu kuazimia,
Muda huwa kama njozi au ndoto ya kutisha:
Afriti na utashi hukutana barazani;
Na hali ya binadamu huwa kama dola ndogo
Hutendewa kama kwamba kumetokea maasi.

(*Lukio anarudi tena*)

LUKIO: Bwana, nduguyo, Kasio, ndiye yuko mlangoni.
Anapenda akuone.

BURUTO: Yu pekee?

LUKIO: La, bwana wangu, anao wengine pamoja naye.

BURUTO: Wawajua?

LUKIO: La, bwana, kofia zao zafika masikioni,
Na nusu ya nyuso zao imefichwa kwa majoho,
Na kwa hiyo sikuweza kuwatambua kwa nyuso.

BURUTO: Kawakaribishe waje.

(*Lukio anatoka*)

Ndiyo wale wafitini. A, fitina, na usiku
Waona haya kutoa uso wako wa hatari
Ambapo maovu yote ni huru? Basi mchana
Utapata wapi pango lenye giza la kutosha
Kuficha surayo mbaya? 'Silitafute, fitina;
Ifiche katika cheko na katika ukunjufu:

Kwani ukitoka nje na surayo ya asili
Hata huko Jehenamu kwenyewe hakuna giza
La kuweza kukuficha hata usitambulike.

(*Wanaingia Kasio, Kasika, Desio, Sinna, Metello Simberi na Tirebonio*)

KASIO: Pengine twakuharibia mapumziko yako:
U hali gani, Buruto? Vipi, tunakubughudhi?
BURUTO: Niko macho mpaka sasa; kucha nzima sijalala.
Je, nawajua mabwana hawa ulokuja nao?
KASIO: Naam, kila mmoja; na hapana mtu hapa
Ambaye hakuheshimu; na kila mmoja wao
Angependa ujione kila Mrumi hashamu
Anavyokufikiria. Huyu ni Tirebonio.
BURUTO: Anakaribishwa hapa.
KASIO: Huyu, Desio Buruto.
BURUTO: Anakaribishwa pia.
KASIO: Huyu, Kasika; huyu, Sinna; na Metello Simberi.
BURUTO: Wote wanakaribishwa. Je, kuna shughuli gani,
Zinazowazuieni kuuona usingizi?
KASIO: Twaweza kusema kando?

(*Buruto na Kasio wananong'ona*)

DESIO: Mashariki iko huku: mapambazuko si huku?
KASIKA: La!
SINNA: A, niwie radhi, bwana, mapambazuko ni huku;
Na miraba ya kijivu ile itiayo rangi
Kwenye mbingu ni risala kuonya mapambazuko.
KASIKA: Wote mtakiri kwamba mmedanganyika sana,
Huku ninakoonyesha kwa upanga wangu ndiko
Jua linakotokea; na ambako ni karibu
Hasa na kusini mwaka mpya ukaribiapo.
Miezi miwili tangu sasa jua litatoka
Kwa juu zaidi kuelekea kaskazini,
Na mashariki ni hapa, sawa na Baraza Kuu.
BURUTO: Nipeni tena mikono yenu mmoja mmoja.

KASIO: Na tuapizane, basi, kwa hii azima yetu.
BURUTO: La, pasiwe na kiapo: ikiwa nyuso za watu,
Mateso ya nyoyo zetu, taabu za siku hizi, –
Kama ni sababu duni, basi nyote sambaeni,
Na kila mtu arudi hima kitandani kwake.
Na dhuluma kuu hii acheni iendelee
Mpaka kila mtu afe zamu yake ikifika.
Bali kama mambo haya, kama ninavyoamini,
Yana moto wa kutosha kuwachemsha waoga
Na kuipa ushujaa mioyo ya wanawake,
Basi, wananchi wenzi, kwa nini tukihitaji
Kitu cho chote zaidi ya nia zetu wenyewe
Kutupa moyo wa ari ya kuondoa dhuluma?
Twahitaji kamba gani inayoishinda njama
Ya Warumi wal'okwisha kutoa kauli yao
Na hawatarudi nyuma? Na kuna kiapo gani
Kinachozidi mwafaka wa imani na imani,
Kwamba hili litakuwa na tuko tayari kufa?
Waapishe makasisi na waoga na waongo,
Na mizoga goigoi iliyooza zamani,
Na wagonjwa wa rohoni wakubalio maovu;
Apisha kwa nia mbaya wale was'oaminika:
Ila usitie ila tendo letu safi hili,
Wala hii ari yetu is'oweza kupoozwa,
Kwa kudhani kuwa nia yetu au tendo letu
Lilihitaji kiapo; kumbe kila tone moja
La damu aliyo nayo Mrumi na kitukufu,
Litakuwa limefanya makosa makubwa sana
Kama atavunja japo chembe ndogo ya ahadi
Yo yote aliyofanya.
KASIO: Lakini Sisero, naye pia tutamshauri?
Nafikiri atakuwa mwenzetu imara sana.
KASIKA: Tusimwache.
SINA: Naam, tusimwache hata kidogo.

METELLO: Naam, na tumpate, kwa sababu mvi zake
Zitatupa sifa njema kwa watu na kununua
Sauti zitazoweza kusifu matendo yetu.
Itasemekana kuwa ni busara yake yeye
Ndiyo iliyoamuru mikono yetu kutenda;
Ujana na ushupavu wetu haut'onekana,
Kwani wote utafichwa na utaratibu wake.
BURUTO: A, msimtaje yeye! Na tusimwambie kitu;
Kwani ni mtu ambaye hawezi kulifuata
Jambo lo lote ambalo limeanzwa na wengine.
KASIO: Basi, yeye natumwache.
KASIKA: Kusema kweli, hafai.
DESIO: Mwinginewe hataguswa, ila ni Kaizari tu?
KASIO: Ni swali zuri, Desio. Nadhani haitafaa
Kuwa Mariko Antoni, kipenzi cha Kaizari,
Aendelee kuishi, baada ya Kaizari:
Tutakuja kugundua kwamba ana ukorofi;
Na, wajua hila zake, akijazitengeneza,
Zaweza kutosheleza kutudhuru sisi sote;
Na njia ya kuzuia ni kumwua Antonio,
Pamoja na Kaizari.
BURUTO: Tutakuwa wakatili mno, Kuyusi Kasio,
Kutoa kichwa, halafu, kukatakata viungo,—
Kama ghadhabu kifoni na kisasi baadaye;
Antonio hakizidi kiungo cha Kaizari:
Na tuwe watambikaji, si makatili, Kayusi.
Sote tusichokipenda ni nia ya Kaizari,
Na nia ya binadamu siyo kitu chenye damu;
Laiti tungefikia nia yake Kaizari,
Bila ya kulazimika kumdhuru Kaizari!
Walakini, ole wake, hana budi atakufa!
Tena, rafiki wapole, na tumwue kishujaa,
Bali siyo kwa ghadhabu; tumwandae kama kombe
La kuwalisha miungu; siyo kumkatakata

Kama zoga lifaalo kuyatupia majibwa:
Mioyo yetu na iwe kama mabwana werevu,
Kuchochea watumishi wakatenda ya ghadhabu
Na halafu iwe kama kwamba inawashutumu.
Itafanya tendo letu la faradhi, si la wivu.
Tutaitwa watakasi, si wauaji waovu.
Bali Mariko Antoni, mwondoeni akilini;
Kwani hawezi kuzidi mkono wa Kaizari
Kichwa chake Kaizari kikisha kuondolewa.

KASIO: Ila nina hofu naye, maana mapenzi yake
Apendayo Kaizari—

BURUTO: Salale, Kasio mwema, 'simtie akilini!
Ikiwa anampenda Kaizari hiariye:
Analoweza kufanya ni kuwaza amfie:
Na hilo kwake ni mno; ni mtu mpenda raha;
Apenda mno michezo, na upuzi na anasa.

TIREBONIO: Hana cha kutuogofya. Yeye natumwache hai;
Kwani ataishi hata alicheke jambo hili.

(*Saa inagonga*)

BURUTO: Kimya! Hesabuni saa.

KASIO: Imegonga mara tatu.

TIREBONIO: Inafaa tuachane.

KASIO: Ila haijulikani,
Kama leo Kaizari atakuja au haji.
Kwa sababu siku hizi kajawa ushirikina,
Ameiacha kabisa imaniye ya zamani,
Juu ya njozi na ndoto na mambo ya kubashiri:
Basi, inawezekana ishara hizi za wazi,
Vitisho vigeni hivi vya usiku huu leo,
Na kushawishishawishi kwa wapiga bao wake
Kwaweza kumzuia kuja Barazani leo.

DESIO: Usiyahofie hayo: akikusudia hivyo
Naweza kumgeuza; anapenda kusikia
Kuwa farasi wa mwitu husalitiwa kwa miti,

Na madubu kwa vioo; kina tembo kwa mashimo,
Akina simba kwa nyavu, watu kwa warairai;
Bali ninapomwambia hapendi warairai,
Hukubali – kwani huwa karaiwa karaika.
N'acheni nifanye kazi, kwa sababu ninaweza
Kuuchezea unyonge wake kwa urairai
Nimlete Barazani.

KASIO: Hasha, tutafuatana, tumlete kwa pamoja.

BURUTO: Iwe kwenye saa mbili: isipite hapo, sivyo?

SINNA: Isipite saa mbili, wala msikose, basi.

METELLO: Na Kayusi Ligario hampendi Kaizari
Kwani alimkemea kwa kumsifia Pompe:
Nashangaa kati yetu hako aliyemtaja!

BURUTO: Tazama, Metello mwema, nenda kamf'ate kwake:
Yeye anipenda sana, na nimempa sababu;
Kamwambie aje hapa, mimi nitamshawishi.

KASIO: Macheo yametukuta: tutakuacha, Buruto: –
Na, rafiki, sambaeni; lakini yakumbukeni
Yale mliyoyasema, na muwe Warumi kweli.

BURUTO: Waungwana watukufu, furahini kwa vicheko;
Msiache nyuso zetu zionyeshe nia yetu,
Lakini tuisitiri, kama vile wafanyavyo
Warumi wetu wachezi, kwa mioyo mitulivu,
Na hali ya kawaida. Basi, nyote kwa herini.

(*Wanaondoka wote ila Buruto*)

Kijana! Lukio! umelala kabisa? Si kitu.
Faidi umande wa asali nzito ya kulala:
Wewe huna ndoto wala njozi ambazo taabu
Na mashaka huzileta katika mbongo za watu:
Ndiyo ma'na umeweza kulala fofofo hivyo.

(*Aingia Poshia*)

POSHIA: Buruto, seyyid yangu!

BURUTO: Poshia, ma'nake nini? Kitu gani chakufanya
Kuamka saa hizi? Si vema kwa afya yako

Kuihatarisha hivi haliyo ya udhaifu
Katika baridi kali hii ya alfajiri.
POSHIA: Wala si vema kwa yako. Buruto, bila upole,
Wewe umenitoroka na kun'acha kitandani.
Na jana usiku kwenye chakula cha magharibi
Ulisimama ghafla na kuanza kutembea
Ukiwaza na kuhema, na mikono umekunja;
Nilipokuliza kisa ulinitolea macho:
Nikakuuliza tena; ukajirarua kichwa
Na kupiga guu chini kwa hasira na ghadhabu:
Lakini nikakazana, na wala hukunijibu;
Ila kwa ghadhabu sana ukapungia mkono
Kunionya niondoke: na mimi nikaondoka;
Kwa sababu sikutaka kukuzidisha ghadhabu
Iloonekana kuwa imesha zidi kiasi.
Tena nilidhani kuwa ni sumbuko la moyo tu,
Ambalo mara kwa mara humpata kila mume.
Halikuachi ukala, au ukazungumza,
Halikuachi kulala; na kama lingaliweza
Kubadili sura yako, kama lilivyobadili
Tabia yako, Buruto, nisingalikutambua.
Seyyid yangu mpenzi, tafadhali nijulishe
Kisa cha huzuni yako.
BURUTO: Ni hali ya afya yangu; ni kwa sababu naumwa.
POSHIA: Buruto ana busara, angekuwa anaumwa,
Angejua la kufanya kurudisha afya yake.
BURUTO: Hivyo ndivyo nifanyavyo. Poshia mwema, kalale.
POSHIA: Buruto kawa mgonjwa? Na dawa ni kutembea
Pasipo kujifunika akusanye ubaridi
Wa usiku wa unyevu? Je, Buruto ni mgonjwa,
Basi atakitoroka kitanda chake kizuri
Na kuijaribu sumu mbaya ya usiku huu,
Na kuichokoza hewa ya unyevu na uchafu
Ajiongeze ugonjwa? La, hasha, Buruto wangu,

Una jambo zito sana katika kifua chako,
Ambalo kwa sababu ya hali na pahali pangu
Nina haki kulijua: nakupigia magoti,
Kwa huo uzuri wangu ulosifika zamani,
Kwa nadhiri zako zote za mapenzi, na nadhiri
Kubwa iliyotuunga ikatufanya mmoja,
Nakusihi unambie niliye wewe mwenyewe,
Niliye wewe mwingine, kwa nini una huzuni
Na ni watu gani leo usiku wal'okufata:
Kwani kumekuja leo watu sita au saba
Hapa, wal'ozifunika nyuso zao hata giza
Lisiweze kuziona.

BURUTO: Tafadhali, sipige magoti, Poshia mpole.

POSHIA: Nisingelazimika, ungekuwa Buruto mpole.
Nambie, Buruto, hivi kwenye nadhiri ya ndoa
Imesemwa nisijue siri zinazokuhusu?
Kumbe mimi ndiyo wewe kama nusunusu tu?
Kukaa nawe mezani, kukupozea kitanda,
Na kuzungumza nawe mara fulani fulani?
Hivi niko pembeni tu katika mapenzi yako?
Basi kama hivyo ndivyo - hapana kinachozidi
Poshia ni kahaba tu siyo mke wa Buruto.

BURUTO: U mke wangu wa kweli, mwaminifu mtukufu;
U mpenzi kwangu kama hayo matone mekundu
Yaingiayo katika moyo wangu wa huzuni.

POSHIA: Kama ingekuwa hivyo ningejua siri hii.
Nakiri ni mwanamke; lakini ni mwanamke
Ambaye Buruto bora kamfanya kuwa mke:
Nakiri ni mwanamke; lakini ni mwanamke
Mwenye sifa kubwa sana – mwanamke binti Kato.
Basi unadhani mtu niliyezaliwa hivyo
Na nikaolewa hivyo, sijazidi kike changu?
Nambie mashauriyo, nami siyatoi nje:
Nimethibitisha sana ustahimili wangu

Kwa kujikata kusudi jeraha hili pajani.
Je, naweza kuhimili hili kwa uvumilivu,
Ila siri za bwanangu nishindwe kuzihimili?

BURUTO: O, enyi miungu nyie,
Nistahilisheni kwa mke mtukufu huyu!

(*Hodi kwa ndani*)

Sikiliza! Kuna hodi: hebu kwanza nenda ndani,
Na halafu moyo wako utazishiriki siri
Za wangu wenye huzuni: Hebu niache haraka

(*Poshia anaondoka*)

Lukio, ni nani apigaye hodi mlangoni?

(*Wanaingia tena Lukio na Ligario*)

LUKIO: Mgonjwa huyu anataka mzungumze naye.

BURUTO: Kayusi Ligario, aliyetajwa na Metello –
Kijana, simama kando – Je, Kayusi Ligario,
Hali gani?

LIGARIO: Zipokee salamu za ulimi wangu dhaifu.

BURUTO: Lo, wakati gani huu, we Ligario shujaa,
Ambao umechagua kujivisha kitambaa!
Laiti usingekuwa mgonjwa hivi ulivyo.

LIGARIO: Mimi si mgonjwa hasha, kama Buruto anayo
Kazi yo yote muhimu yenye jina la heshima.

BURUTO: Nina kazi kama hiyo usemayo, Ligario,
Ungekuwa na sikio lenye afya lisikie.

LIGARIO: Kwa hiyo miungu yote Warumi waabuduyo,
Nautupilia mbali ugonjwa nilio nao.
E, wewe roho ya Roma! Shujaa mwana wa watu!
Mwana shujaa mzawa wa nyumba tukufu sana!
Umekuwa kama bingwa mpungiaji wa pepo,
Na umenirudishia afia yangu dhaifu:
Niamuru nikimbie, nitaweza kushindana
Na visivyowezekana; naam, na nivishinde.
Je, unayo kazi gani, inohitaji kufanywa?

BURUTO: Kazi itakayofanya wagonjwa kuwa wazima.

LIGARIO: Je, hakuna wengineo walio sasa wazima,
Ambao hatuna budi ya kuwafanya wagonjwa?
BURUTO: Hivyo tutafanya pia. Yenyewe, Kayusi wangu,
Nitakwelezayo hapo tutapokuwa njiani,
Tukienda kwake huyo atotendwa kazi hiyo.
LIGARIO: Basi wewe tangulia, na mimi kwa moyo mpya
Nitafuata kutenda jambo nisilolijua;
Bali yatosha kujua naongozwa na Buruto.
BURUTO: Haya, nifuate basi.
(*Wanaondoka*)

Onyesho la II: Chumbani, Nyumbani mwa Kaizari

(*Ngurumo na Umeme. Aingia Kaizari, kavaa nguo za usiku*)
KAIZARI: Leo mbingu wala nchi haikuwa na amani:
Mara tatu Kapunia kalia usingizini,
'Yala, wanamwua Kaizari!' Kuna nani ndani?
(*Aingia Mtumishi*)
MTUMISHI: Naam, seyyid yangu!
KAIZARI: Nenda ukawaambie watabiri watambike,
Walete maoni yao juu ya mafanikio.
MTUMISHI: Ee walla, bwana wangu.
(*Mtumishi anatoka*)
(*Aingia Kapunia*)
KAPUNIA: Una nini, Kaizari? Wakusudia kutoka?
Leo hutatoka kamwe, utashinda papa hapa.
KAIZARI: Kaizari atatoka: vitu vilivyonitisha
Havijaniona uso, vimeniona mgongo;
Vionapo uso wangu vitatoweka haraka.
KAPUNIA: Kaizari, sijajali fali; sasa zanitisha.
Kuna mtu hapa ndani, anayesema ya kuwa,
Kuacha tuliyoona na tuliyoyasikia,
Kuna mambo ya kutisha aliyoona mlinda.
Anasema simba jike kazaa barabarani;
Kaburi zimefunguka watu wafu wakatoka;

Askari wa kutisha, waliopangwa vizuri,
Kwa safu na kwa vikosi, kawaida ya kivita,
Wamepigana mbinguni, damu ikalinyeshea
Jumba la Baraza Kuu. Na kelele za kivita
Ziligongana hewani, na farasi walilia,
Na watu waliokuwa wakifa wakaugua;
Na roho za marehemu zikalia majiani.
Kaizari, mambo hayo si mambo ya kawaida,
Na tena yananitisha!

KAIZARI: Nini chaweza epukwa ambacho hatima yake
Imekwisha dhamiriwa na miungu wenye ezi?
Walakini hata hivyo Kaizari atatoka;
Maana maonyo haya ni kwake na kwa wengine.

KAPUNIA: Fukara wanapokufa vimwondo havimuliki;
Bali na mbingu hunadi kifo chake mfalme.

KAIZARI: W'oga hufa mara nyingi kabla ya vifo vyao;
Mashujaa hawaonji kifo ila mara moja.
Kati ya vioja vyote nilivyokwisha sikia,
Kishangazacho zaidi ni woga wa binadamu.
Kwani kifo, kwa sababu ni hatima ya lazima,
Bila shaka kitakuja siku itakapotimu.

(*Mtumishi anaingia tena*)

Watabiri wasemaje?

MTUMISHI: Wasema wasingependa utoke nyumbani leo.
Mhanga wal'opasua haukuwa una moyo.

KAIZARI: Miungu hufanya hayo kufedhehesha waoga:
Kaizari atakuwa nyama asiye na moyo
Akishinda hapo leo kwa sababu ya uoga.
La, Kaizari hawezi. Hatari yajua kuwa
Kaizari ni hatari inayozidi hatari,
Sisi ni simba wawili wazaliwa siku moja,
Nami nilitangulia, na ni mkali zaidi:
Kaizari atatoka.

KAPUNIA: Ole wako, bwana wangu.

Busarayo imeshia kwenye ushupavu wako.
Usitoke nje leo: sema kuwa woga wangu
Ndio unokushindisha nyumbani, si woga wako.
Tutamtuma Mariko Antonio Barazani
Na atasema ya kwamba haliyo si njema leo:
Tafadhali nisikie, nakupigia magoti.

KAIZARI: Antonio atakwenda aseme kuwa naumwa;
Nami kwa kukupendeza sitaondoka nyumbani.

(*Aingia Desio*)

Huyu hapa Desio Buruto, atawaambia.

DESIO: Kaizari, salaam! Habari za asubuhi,
Kaizari mtukufu? Unaitwa Barazani.

KAIZARI: Na umekuja wakati unaopendeza sana,
Ili uwapelekee salamu zangu wajumbe,
Kawaambie ya kuwa sitaweza kuja leo:
Sitaweza, ni uwongo; sithubutu, unazidi:
Kawaambie, Desio, kuwa sitakuja leo.

KAPUNIA: Kaseme kuwa aumwa.

KAIZARI: Kaizari aongope?
Niunyoshe ushindini mkono wangu vitani,
Kisha nisiseme kweli kwa vizee vyenye mvi?
Desio, kawaambie Kaizari hatakuja.

DESIO: Kaizari, mwenye enzi, nambie sababu moja,
Nisije nikazomewa nita'powambia hivyo.

KAIZARI: Sababu ni kwamba siji,—i katika nia yangu.
Hiyo inatosheleza kuwaridhisha Wabunge.
Walakini kwa sababu ya kukuridhisha wewe,
Kwa sababu nakupenda, basi nitakujulisha.
Mke wangu, Kapunia, huyu, hataki nitoke.
Kaota usiku kwamba kaona sanamu yangu
Mithili ya chemichemi iliyo na vinywa mia,
Ilitema damu safi; na Warumi wenye nguvu
Wakaja wakifurahi, na kunawa hiyo damu.
Na hii asema kuwa ni maonyo na ishara

Ya maovu yanokuja: naye kapiga magoti
Na kuniomba ya kuwa nishinde nyumbani leo.

DESIO: Ndoto hii, Kaizari imebashiriwa sivyo;
Ilikuwa ni ishara nzuri na yenye bahati.
Sanamu kutoka damu katika sehemu nyingi,
Ambayo Warumi wengi walinawa kwa furaha,
Kunaonyesha ya kwamba kwa kutokana na wewe
Roma kuu itanyonya damu ya uzima mpya,
Na kwamba watu wakubwa watakuja kusongana
Kutaka dawa, mawaa, kumbukumbu na nishani.
Hiyo ndiyo tafsiri ya ndoto ya Kapunia.

KAIZARI: Na ulivyoifasiri ndivyo hususa ilivyo.

DESIO: Na hasa utapojua yale nitakayosema—
Basi yafaa ujue: Bunge limesha amua
Kumvisha taji leo Kaizari mwenye enzi.
Ukipeleka habari kwamba leo hutakwenda,
Hwenda wabadili nia. Tena, zaidi ya hayo,
Itakuwa kichekesho, mtu kuweza kusema,
Vunjeni Baraza Kuu mpaka siku nyingineyo
Mke wake Kaizari atapoweza kuota
Ndoto inayopendeza. Kaizari ajifiche,
Je, hawatanong'ona, 'Lo, Kaizari kaogopa?'
Nisamehe, Kaizari, kwani pendo langu kwako
Lanilazimisha mimi niyaseme mambo haya,
Na akili zangu mimi zinatii pendo langu.

KAIZARI: Haya sasa, Kapunia, zitazame hofu zako,
Zionekanavyo kuwa ni za kijinga kabisa!
Naona aibu sana kwamba nilishawishika.
Haya, nipe joho langu, kwa sababu nitakwenda: –

(*Wanaingia Pubulio, Buruto, Ligario, Metello, Kasika Tirebonio na Sinna*)

Na tazama, Pubulio huyu kaja kuniita.

PUBULIO: Sabalkheri, Kaizari?

KAIZARI: Karibu, Pubulio.

Lo, Buruto, hata wewe umejidamka hivi?
Sabalkheri, Kasika. Na Kayusi Ligario
Kaizari hajapata akawa adui yako
Sawa na maradhi haya yakukondeshayo hivi.
Saa ngapi?

BURUTO: Kaizari, imegonga saa mbili.

KAIZARI: Nakushukuru kwa taabu na uungwana wako.

(*Aingia Antonio*)

Ona, hata Antonio akeshaye kwa sherehe,
Naye piya kaamka. Baraka za asubuhi,
Antonio!

ANTONIO: Ziweko na kwako pia, mtukufu Kaizari.

KAIZARI: Kawaambieni huko ndani wajitayarishe.
Mwenye lawama ni mimi kwa kungojelewa hivi.
Una hali gani, Sinna? Metello, u hali gani?
Na wewe, Terebonio! Nitapata saa nzima,
Ya kuzungumza nawe: njoo tuonane leo:
Kuwa karibu na mimi niweze kukukumbuka.

TIREBONIO: Ee walla, Kaizari (*Kando*) nitakuwa karibu mno
Hata rafikizo bora watamani niwe mbali.

KAIZARI: Rafiki wema, nendeni ndani mkanywe vinywaji
Kidogo pamoja nami, na kisha, kama rafiki,
Tutaondoka pamoja.

BURUTO: (*kando*) Moyo huu wa Buruto unalia, Kaizari,
Kwa kutafakari kwamba kuwa kama siyo kuwa.

(*Wanatoka*)

Onyesho la III: Barabarani. Karibu na Jumba Kuu la Serikali

(*Aingia Aritemidoro akisoma karatasi*)

ARITEMIDORO: Kaizari jihadhari na Buruto; mwangalie Kasio; usimkaribie Kasika; mtupie jicho Sinna; usimwamini Tirebonio; mwangalie sana Metello Simberi Desio Buruto hakupendi: umemkosea Kayusi Ligario. Watu wote hawa wana nia moja tu, nayo haimpendi

Kaizari. Kama wewe si mtu wa kuishi milele,
jilinde: ushupavu ukizidi huleta uhaini.
Miungu wenyezi na wakulinde. Akupendaye-ARITEMIDORO'
Tasimama hapa hadi Kaizari apitapo,
Tajifanya mhitaji nimpe barua hii.
Moyo wangu unalia vile wema hauwezi
Kuepa meno ya wivu. Pindi ukisoma hii,
Kaizari, unaweza ukapona: kama sivyo.
Nyota yako ina njama pamoja na mahaini.

Onyesho la IV: Sehemu nyingine ya barabarani, mbele ya nyumba ya Buruto

(*Wanaingia Poshia na Lukio*)

POSHIA: Tafadhali, bwana mdogo, nenda hima Barazani;
Usingoje kunijibu, bali nenda hima hima:
Unangoja kitu gani?
LUKIO: Kujua n'tumwalo, mama.
POSHIA: Ni heri ungalikwenda kule na kurudi hapa
Kabla sijakwambia ukafanye nini kule.
(*Kando*). O, uthabiti wa moyo, kuwa mathubuti kwangu!
Tenga kwa jilima kubwa moyo na ulimi wangu!
Nina moyo wa kiume na nguvu za mwanamke.
Ni shida kwa mwanamke kuweza kuweka siri!
Bado ukingali hapa?
LUKIO: Bibie, niende kule nikafanye jambo gani?
Nende mbio Barazani, basi, hakuna zaidi?
Halafu nirudi kwako, basi, hakuna zaidi?
POSHIA: Naam, enenda, baba, kaniletee habari
Kama bwanako hajambo, kwani alipoondoka
Alikuwa anaumwa; tena angalia vema
Afanyalo Kaizari, wahitaji wamwonao.
Hebu, sikiliza, baba, ni kelele gani hiyo?
LUKIO: Siisikii, bibie.
POSHIA: Tafadhali sikiliza. Nazisikia ghasia

Za kelele kama kwamba ni ghasia za ugomvi,
Na upepo wazileta kutokea Barazani.

LUKIO: Kwa kweli mimi, bibie, sikisikii cho chote.

(*Aingia Mtabiri*)

POSHIA: Njoo hapa, wewe: ulikuwa wapi?

MTABIRI: Nyumbani kwangu, bibie mwema.

POSHIA: Hivi saa ngapi sasa?

MTABIRI: Yakaribia saa tatu, bibie.

POSHIA: Kaizari kesha kwenda Barazani au bado?

MTABIRI: Bado, bibie: ninakwenda kusimama pahali
Pangu nimwone atapopita kwenda Barazani.

POSHIA: Una ombi lo lote kwa Kaizari ama sivyo?

MTABIRI: Naam, ninalo bibie, akinisikiliza;
Tamwambia ajifanye rafiki yake mwenyewe.

POSHIA: Wajua dhara lo lote ambalo akusudiwa?

MTABIRI: Sijui dhara lo lote ambalo litatokea,
Lakini najua mengi yawezayo kutokea.
Kwa heri. Pahali hapa barabara ni nyembamba:
Umati umwandamao Kaizari, wa wajumbe,
Mawaziri na raia wahitaji unaweza
Ukamsonga mnyonge nusura ya kumuua.
Nitajibanza pembeni, pahala penye nafasi,
Na kusema naye hapo Kaizari mtukufu,
Atapokuwa apita.

(*Mtabiri anatoka*)

POSHIA: Lazima niende ndani (*kando*). A, moyo wa mwanamke,
Kweli ni kitu dhaifu! Ole wangu, O, Buruto,
Miungu ikuongoze katika shughuli yako!
Kijana kanisikia—Buruto analo ombi,
Kaizari halikidhi. – O, nataka kuzimia.
Haya, kimbia, Lukio, kamsalimu bwanangu;
Mwambie nina furaha; kisha rudi unambie,
Lile atalokwambia.

(*Wanatoka mmoja mmoja*)

III

Onyesho la I: Mbele ya Baraza Kuu

(*Wajumbe wako juu. Kundi la watu barabarani linaelekea Baraza Kuu. Miongoni mwao yumo Aritemidoro na Mtabiri. Tarumbeta.*

Wanaingia Kaizari, Buruto, Kasio, Kasika, Desio, Metello, Tirebonio, Sinna, Antonio, Lepido, Popilio, Pubulio, na wengineo)

KAIZARI: (*Kwa* Mtabiri) Tarehe ya katikati ya Machi
imesha fika.
MTABIRI: Hivyo ndivyo, Kaizari, lakini haijapita.
ARITEMIDORO: Salaam, Kaizari! Soma maandiko haya.
DESIO: Tirebonio aomba utapopata nafasi
Ulisome ombi lake hili la unyenyekevu.
ARITEMIDORO: Tafadhali, Kaizari, soma ombi langu kwanza,
Kwani linayemhusu ni Kaizari mwenyewe,
Kwa hiyo, basi, lisome, Kaizari mtukufu.
KAIZARI: Linalotuhusu sisi litaangaliwa mwisho.
ARITEMIDORO: 'Sichelewe, Kaizari; ulisome sasa hivi.
KAIZARI: Je, mtu huyu kichaa?
PUBULIO: Simile, mpuzi wee!
KASIO: Kwa nini maombi yako watoa barabarani?
Yapeleke Barazani.

(*Kaizari anakwenda kwenye Baraza Kuu: wengine wanafuata*)

POPILIO: Naitakia fanaka shughuli yenu ya leo.
KASIO: Shughuli gani, Popilio?

POPILIO: Kwa herini.
(Anamwendea Kaizari)
BURUTO: Popilio kasemaje?.
KASIO: Aitakia fanaka shughuli yetu ya leo.
Nina hofu nia yetu ime'sha kujulikana.
BURUTO: Ona anavyomwendea Kaizari: mtazame.
KASIO: Kasika, usichelewe, twahofu kugunduliwa.
Buruto, tutafanyaje? Hii ikijulikana,
Mmoja baina yetu, Kasio na Kaizari,
Hatarudi asilani, maana nitajiua.
BURUTO: Kasio, tulia tuli: Yule Popilio Lena,
Hasemei nia yetu; kwani, ona, anacheka,
Na Kaizari kapoa, na wala habadiliki.
KASIO: Tirebonio ajua saa yake; kwani, ona,
Buruto, anamuondoa Mariko Antonio.
(Antonio na Tirebonio wanaondoka)
(Kaizari na Wabunge wanakaa)
DESIO: Wapi Metello Simberi? Yeye na aende sasa,
Atoe maombi yake mbele yake Kaizari.
BURUTO: Yuko tayari: sogea karibu umwunge mkono.
SINNA: Kasika, uwe wa kwanza kwinua mkono wako.
KAIZARI: Je, wote mko tayari? Kuna nini kumpasa
Kaizari na Baraza lake kukitengeneza?
METELLO: Mtukufu, mwenye nguvu, mwenye enzi, Kaizari,
Metello Simberi hapa atupa kitini pako,
Moyo wa unyenyekevu—
KAIZARI: Inanibidi nikuzuie, Metello Simberi.
Kuinamanama huku na staha hizi za chini
Zinaweza kuchemsha damu za watu wa ovyo,
Na kugeuza kanuni na sheria za asili
Ziwe sheria za wana. Bali usidanganyike,
Na kudhani Kaizari ana damu ya uasi,
Iwezayo kuyeyushwa iache asili yake,
Kwa mambo yanayoweza kuyeyusha wapumbavu;

Ya'ni maneno matamu, heshima za kuinama,
Au kujipendekeza kwa uwongo kama mbwa.
Ndugu yako kahamishwa kwa mujibu wa sheria:
Kama, basi, wainama, wasali na kujibemba,
Kwa ajili yake yeye, mimi nakupiga teke,
Jinsi apigwavyo mbwa, uondoke mbele yangu.
Fahamu kuwa daima Kaizari hakosei,
Naye habadili nia kama hapana sababu.
METELLO: Hapana sauti hapa inopendeza zaidi
Kuliko sauti yangu, itakayonisemea,
Na kuridhisha sikio la Kaizari mkuu,
Ili akasamehewa ndugu aliyehamishwa?
BURUTO: Nabusu mkono wako, bali si kwa ulaghai,
Kaizari, nikiomba Pubulio wa Simberi
Aachiwe huru, mara.
KAIZARI: Nini, Buruto!
KASIO: Msamaha Kaizari; Kaizari, msamaha!
Kasio anaanguka chini ya miguu yako,
Na kumwombea uhuru Pubulio wa Simberi.
KAIZARI: Ningekuwa kama wewe, ninge'za kushawishika.
Ningeshawishi kwa sala, sala zingenishawishi:
Bali mimi ni imara kama nyota ya shemali,
Il'o na hali ya kweli, imara yenye kituo,
Wala haina kifani huko kote uwinguni.
Uwingu umepambika kwa nyota bila idadi,
Ambazo zote ni moto na zote hutoa nuru;
Bali kuna nyota moja miongoni mwazo zote
Ikaayo pale pale.
Na dunia kadhalika ina watu wengi sana,
Nao wote wana mwili, wana damu na akili:
Bali miongoni mwao namjua mmoja tu
Ambaye hakanushiki, hukamata pale pale,
Na wala hatikisiki: na mtu huyo ni mimi,
Nitaonyesha kidogo, angao kwa jambo hili-

Niliamuru imara kuhamishwa kwa Simberi,
Na bado niko imara abakie huko huko.
SINNA: O, Kaizari –
KAIZARI: Toka hapa! Unaweza kuinua Olimpio?
DESIO: Kaizari mkuu –
KAIZARI: Hata Buruto mwenyewe hapigi magoti bure?
KASIKA: Nisemeeni, mikono!
(*Kasika anamchoma Kaizari shingoni. Halafu anachomwa na mahaini wengine, na Mariko Buruto mwishoni*)
KAIZARI: Hata na wewe, Buruto? Basi, kugwa, Kaizari.
(*Anakufa. Wajumbe na raia wanatoka wamepigwa na bumbuazi*)
SINNA: Uhuru! Uhuru sasa! Udhalimu umekufa!
Kimbieni, tangazeni, kote, mabarabarani!
KASIO: Wengine majukwaani, wapige kelele huko,
'Uhuru! Uhuru! Uraia!'
BURUTO: Wananchi na wajumbe, msihofu, tulieni;
Deni la kupenda cheo, sasa limekwisha lipwa.
KASIKA: Wewe nenda ukapande kwenye jukwaa, Buruto.
DESIO: Na Kasio kadhalika.
BURUTO: Pubulio yuko wapi?
SINNA: Huyu hapa, kaduazwa sana na maasi haya.
METELLO: Simameni kwa pamoja, ili rafiki fulani
Wa Kaizari—
BURUTO: Usitaje kusimama. Pubulio, changamka;
Hapana dhara lo lote lanuiwa juu yako
Au Mrumi ye yote; waambie Pubulio.
KASIO: Kisha twache, Pubulio, watu wasituvamie,
Na kudhuru mvi zako.
BURUTO: Sawa sawa, fanya hivyo: ye yote asidhurike,
Kwa kitendo chetu hiki, ila si tuliokitenda.
(*Pubulio anaondoka*)
(*Tirebonio anarudi*)
KASIO: Antonio yuko wapi?

TIREBONIO: Kakimbilia nyumbani kwake huku kaduwaa:
Wanaume, wanawake na watoto washangaa,
Walia na kukimbia kama kwamba ni kiama.
BURUTO: Miungu, tuko tayari kujua matakwa yenu:
Twafahamu tutakufa: wakati na kusubiri
Ndivyo husumbua watu.
KASIO: Na mpunguza miaka ishirini ya uhai,
Apunguza hiyo hiyo ya kuogopa mauti.
BURUTO: Ukisha kubali hayo, kifo, basi, ni fadhila:
Nasi tuloufupisha muda wake Kaizari,
Wa kuogopa mauti tumemtendea mema.
Inameni, Wananchi, inamieni Warumi,
Tuinawe mikononi, damu yake Kaizari,
Hadi juu kwenye viko, na kupaka panga zetu:
Kisha twendeni sokoni, na kuzipunga vichwani
Panga zetu zenye damu, tuzipaaze sauti,
Sote tuseme, 'Amani, Uhuru, na Uungwana!'
KASIO: Inameni, basi na kunawa. Vizazi vingapi
Kutoka hivi sasa, tendo letu bora hili,
Litaigizwaigizwa katika nchi ambazo
Bado hazijazaliwa, na ndimi tusozijua!
BURUTO: Mara ngapi tangu sasa, Kaizari kwa kuchezwa,
Atatoka damu tena, ambaye kwa hivi sasa
Kalala penye kiweko cha Pompe wala hazidi
Japo vumbi kwa thamani!
KASIO: Kila kitapotendeka na hiki kikundi chetu
Kitakumbukwa kiitwe wakomboa nchi yao.
DESIO: Twende zetu?
KASIO: Naam, sote twondoke:
Buruto ataongoza nasi tutamfuata
Kwa nyoyo za kishujaa na bora kwa Roma nzima.
(*Aingia Mtumishi*)
BURUTO: Hebu! N'nani anakuja?
Rafiki wa Antonio.

MTUMISHI: Ni hivi, bwana Buruto, bwana wangu kanituma
Nije nipige magoti; na nisujudie hivi;
Ndivyo Mariko Antoni alivyoniamrisha.
Na nikisha kusujudu kataka niseme hivi:
Buruto ni mtukufu, ni mtu mwenye busara,
Shujaa na mwaminifu; Kaizari alikuwa
Mweza, jasiri, maliki, na mtu mwenye mapenzi.
Ninampenda Buruto tena ninamheshimu;
Sema kuwa Kaizari nilikuwa namwogopa,
Nilikuwa nampenda tena nilimheshimu,
Buruto akikubali Antonio aje kwake
Kwa salama aelezwe jinsi gani Kaizari
Kastahili mauti, Antoni hatampenda
Kaizari marehemu jinsi atavyompenda
Buruto aliye hai; bali ataifuata
Bahati na mambo yote ya Buruto mtukufu,
Katika mashaka haya ya hali iliyo mpya,
Kwa uaminifu safi. Hivyo ndivyo asemavyo
Bwana wangu Antonio.

BURUTO: Bwana wako ni Mrumi wa busara na shujaa;
Kamwe sijamfikiri kuwa yuko vinginevyo.
Kamwambie, akipenda, anaweza kuja hapa;
Naapa, ataelezwa na kuondoka salama.

MTUMISHI: Tamleta sasa hivi.

(*Mtumishi anatoka*)

BURUTO: Najua tutatambua kuwa yu rafiki mwema.

KASIO: Natumai hivyo ndivyo: bali namwogopa sana;
Na mimi mashaka yangu, mara nyingi huwa kweli.

BURUTO: Na Antonio mwenyewe huyu hapa anakuja.

(*Antonio anaingia*)

Karibu, Mariko Antonio.

ANTONIO: A, Kaizari mkuu! Umelala chini hivyo?
Je, ushindi wako wote, utukufu na fahari,
Na mateka vimenywea kiasi hiki? Kwa heri.

Mimi sijui, mabwana, mnakusudia nini,
Nani zaidi kabaki wa kumwagwa damu yake.
Ni nani zaidi bado amejaa mno damu:
Kama ni mimi, hapana saa inostahili
Kama saa Kaizari aliyopata mauti;
Wala hapana silaha yenye nusu ya thamani
Yazo hizo panga zenu zilizotiwa rutuba,
Na damu bora kuliko yote hapa duniani.
Nawatafadhalisheni, ikiwa hamnipendi,
Timizeni nia yenu papa hapa sasa hivi,
Mikono yenu ya damu ingali yatoa moshi.
Japo kama ningaishi miaka elfu moja,
Sitasitahili kufa; wala hapana mahali
Au jinsi ya mauti ambayo nitaipenda,
Sawa na mahali hapa, karibu na Kaizari,
Na kuuawa na ninyi wateule na mabwana,
Wenyi wa wakati huu.

BURUTO: O, Antoni, 'usiombe kwetu sisi kifo chako.
Japo sasa ni lazima tuonekane ni watu
Wenye damu, wakatili kama unavyotuona,
Kwa hii mikono yetu na tendo letu la sasa;
Lakini unachoona ni mikono yetu tu
Na tendo la damu hili ambalo imelitenda:
Nyoyo zetu huzioni – ambazo zina huzuni; –
Na huzuni, kwa sababu ya Roma kudhulumiwa –
Dawa ya moto ni moto, ya huzuni ni huzuni –
Ndiyo iliyomtenda Kaizari tendo hili,
Kwako, wewe Antonio, panga zetu siyo kali;
Mikono yetu, japokuwa ina nguvu za chuki,
Na mioyo yetu ya kidugu, inakupokea
Kwa mapenzi na upole, moyo safi na heshima.

KASIO: Sautiyo itakuwa sawa na ya mwingineo
Wakati utapofika wa kugawa vyeo vipya.

BURUTO: Ila vumilia mpaka kwanza tutulize watu,

Ambao kwa hivi sasa wana hofu kubwa sana,
Halafu tutakweleza sababu ilonifanya
Mimi niliyempenda Kaizari hata pale
Wakati nikimchoma nilitenda nilotenda.

ANTONIO: Mimi sinayo mashaka juu ya busara yako.
Kila mtu na alete mkonowe wenye damu:
Kwanza, Mariko Buruto nitashikana na wewe; –
Kisha Kayusi Kasio, nitaushika wa kwako; –
Sasa, Desio Buruto, wako; na wako Metello;
Wako, Sinna; – na Kasika wangu shujaa, wa kwako;
Na mwisho kabisa, japo si kwa mapenzi, wa kwako,
Tirebonio mpole.
Waungwana, – ole wangu, sijui niseme nini?
Kwaminika kwangu sasa kuko mashakani sana,
Na baina ya maovu mawili hamna budi
Mniwazie mojapo—mwoga au mlaghai.
Ya kwamba nilikupenda, Kaizari, o, ni kweli:
Basi, kama roho yako ikitutazama sasa,
Haitatiwa uchungu kuzidi wa kifo chako,
Kumwona Antoni wako akifanya masilahi,
Akivishika vidole vya damu vya aduizo,
Mtukufu Kaizari, mbele ya maiti yako?
Ningalikuwa na macho sawa na majerahayo,
Yatoe machozi kasi yatoavyo damu yako
Ingelaiki zaidi kuliko kuafikana
Pamwe na adui zako, na kufanya urafiki.
Kunradhi, Juliasi! Hapa walikuzingia
Kama ayala shujaa, na hapa ukaanguka;
Na hapa wawinda wako wasimama na madoa
Ya kushambuliwa kwako na damu ya kifo chako.
A, dunia, ulikuwa msitu wa mwindwa huyu,
Naye kweli, a, dunia, alikuwa moyo wako!
Umelala hapa kama paa aliyeangushwa
Na wawinda wake wengi, watoto wa kifalme.

KASIO: Lo, Mariko Antonio –
ANTONIO: Niwie radhi, Kasio:
Aduize Kaizari watasema mambo haya;
Basi kwa rafiki yake, ni jambo la kawaida.
KASIO: Sikulaumu kwa huko kumsifu Kaizari;
Lakini wakusudia kupatana nini nasi?
Tukutie miongoni mwao marafiki zetu,
Au tujendee zetu tusikutumainie?
ANTONIO: Kwa hiyo niliishika mikono yenu, lakini
Nilivutwa kwa kumwona Kaizari yuko chini.
Ni rafiki yenu wote na nawapendeni nyote;
Kwa matumaini haya, kwamba mtanieleza
Sababu na jinsi yake hatari ya Kaizari.
BURUTO: Kama sivyo tendo hili lilikuwa la kishenzi;
Sababu zetu ni safi, Antonio, ungekuwa
Ni mwanae Kaizari bado zingekuridhisha.
ANTONIO: Wala siombi zaidi, ila naomba ruhusa,
Nitwae maiti yake niyapeleke sokoni,
Na ipasavyo rafiki nisimame jukwaani,
Niweze kuhutubia katika matanga yake.
BURUTO: Utaweza, Antonio.
KASIO: Buruto, hebu tuseme (*kando kwa Buruto*); hujui unalotenda;
Usikubali Mariko Antonio akaseme
Katika matanga yake: wajua kiasi gani
Watu watakavyovutwa kwa yale atayosema?
BURUTO: Tafadhali, kuwa radhi; – mimi nitatangulia
Jukwaani nieleze sababu iliyofanya
Tukamwua Kaizari: na kuwa atayosema
Antonio, atasema kwa idhini na ruhusa;
Pia kuwa tunapenda Kaizari afanyiwe
Ibada na mambo yote yapasayo kisheria.
Kwetu hayo ni faida, hatutapata madhara.
KASIO: Sijui yatayoweza kutokea; siridhiki.

BURUTO: Mariko Antoni, haya, waweza kuyachukua
Maiti ya Kaizari: katika hotuba yako
Ya matanga, 'situsute, bali sema mema yote,
Uwezayo kufikiri kumhusu Kaizari.
Na useme wahutubu kwa ruhusa yetu sisi:
Kama hukubali hivyo hutashiriki kabisa
Katika matanga yake: tena utaposemea
Ni jukwaa lile lile ambako nakwenda sasa,
Ba'da ya hotuba yangu itakapomalizika.
ANTONIO: Itakuwa hivyo, basi: mimi siombi zaidi.
BURUTO: Yatayarishe maiti, basi, na utufuate.
(*Wote wanaondoka ila Antonio*)
ANTONIO: Niwie radhi, e, wewe dongo utokaye damu,
Kwamba nakuwa mpole, na kwamba nakuwa mwema
Na wachinja watu hawa! Wewe ndiyo masalia
Ya binadamu mkuu kupita wengine wote
Waliopata kuishi kwenye wingi wa nyakati.
Ole wa mkono huo ambao umeimwaga
Damu ya thamani hivyo! Nami sasa nabáshiri
Juu ya madonda yako, yafunguayo midomo
Mithili ya vinywa bubu na kuutafadhalisha
Ulimi wangu utoe sautiye na kauli.
Janga litaangukia maungo ya binadamu;
Ghadhabu kali nchini, na vita vya wananchi,
Vitaelemea kila sehemu ya Italia.
Damu na maangamizo vitakuwa kawaida,
Na mambo yanayotisha yatakuwa mazoea,
Kina mama watacheka wakati wanapoona
Vyana vyao vikikatwa kwa mikono ya kitali.
Kuyazoea maovu kutazimisha huruma:
Na roho ya Kaizari ikitafuta kisasi
Bega kwa bega na Ate mkali toka Jahimu,
Kwa sauti ya maliki italia kwa nchini,
"Shari!" na kuachilia majibwa ya mapigano,

Hata tendo ovu hili linuke katika nchi
Kwa uvundo wa mizoga ikililia kuzikwa.
(*Aingia Mtumishi*)
U mtu wa Ottavio Kaizari, ama sivyo?
MTUMISHI: Ndivyo, Bwana Antonio.
ANTONIO: Kaizari andikile kumwagiza aje Roma.
MTUMISHI: Naye alizipokea baruaze na yuaja;
Na amenituma nije nikwambie kwa mdomo –
(*Kwa kuona maiti ya Kaizari*)
O, Kaizari!
ANTONIO: Una huzuni moyoni, nenda kando ukalie.
Kumbe huruma, naona, yaweza kuambukizwa;
Kwa sababu macho yangu kwa kuona hizo shanga
Za huzuni machonimwo, nayo yatoa machozi.
Je, bwanao anakuja?
MTUMISHI: Leo alala maili ishirini na moja tu,
Kutoka mjini Roma.
ANTONIO: Rudi hima umwarifu mambo yaliyotokea:
Hapa kuna Roma yenye msiba, yenye hatari,
Bado haijawa Roma salama kwa Ottavio;
Haya, basi, rudi kwake, umfahamishe hivyo;
Ila subiri kidogo; ngoja kwanza nipeleke
Maiti haya sokoni: huko nitajitahidi
Katika hotuba yangu, kuona jinsi ambavyo
Watu wamelipokea jambo la uovu hili
La watu waovu hawa; halafu utaeleza
Kwa kijana Ottavio mambo yenyewe yalivyo.
Haya, basi, niauni.
(*Wanaondoka na maiti ya Kaizari*)

Onyesho la II: Sokoni

(*Wanaingia Buruto na Kasio na kundi kubwa la raia*)

RAIA: Tutaelezwa sababu: na tuelezwe sababu.
BURUTO: Basi, nifuatieni, msikie, marafiki.

Kasio, wewe enenda kwenye barabara lile,
Kusudi tuyagawanye makundi makubwa haya.
Watakaonisikia na wabaki papa hapa;
Wataomsikiliza Kasio waende naye.
Na sababu za kumwua Kaizari zitasemwa
Waziwazi hadharani.

RAIA 1: 'Tamsikia Buruto.

RAIA 2: Mimi nitamsikia Kasio tulinganishe
Sababu zao ikiwa zitasemwa mbalimbali.

(*Kasio anaondoka na raia wengine, Buruto anapanda kwenye jukwaa*)

RAIA 3: Mtukufu Buruto kapanda: kelele!

BURUTO: Tulieni mpaka mwisho.

Warumi, wananchi na wapenzi! nisikilizeni kwa kisa changu, na nyamazeni ili mweze kusikia: nisadikini kwa sababu ya heshima yangu, na istahini heshima yangu ili mweze kuamini: nihukumuni katika busara yenu, na ziamsheni akili zenu ili mweze kuwa mahakimu hodari. Ikiwa pana mtu ye yote katika umati huu, mtu ye yote rafiki mpenzi wa Kaizari, kwake nasema kwamba mapenzi ya Buruto kwa Kaizari hayakuwa chini ya mapenzi yake yeye. Ikiwa, basi, rafiki mpenzi huyo atauliza kwa nini Buruto kamshambulia Kaizari, jibu langu ni hili:– Siyo kwa sababu sikumpenda sana Kaizari, bali kwa sababu niliipenda Roma zaidi. Je, mngependa Kaizari awe hai na nyinyi wote mfe watumwa, au Kaizari afe na ninyi muishi waungwana? Kwa sababu Kaizari alinipenda, namlilia: kwa sababu alikuwa na sudi, nashangilia; kwa sababu alikuwa shujaa namtukuza: lakini kwa sababu alikuwa mpenda cheo, nimemwua. Pana machozi kwa ajili ya mapenzi yake; shangwe kwa ajili ya sudi; utukufu kwa ajili ya ushujaa; na kifo kwa kupenda cheo kwake. Kuna

dhalili gani hapa ambaye angependa kuwa mtumwa? Kama yupo na aseme, kwani yeye nimemkosea. Kuna mshenzi gani hapa ambaye asingependa kuwa Mrumi? Kama yupo, na aseme; kwani yeye nimemkosea. Kuna nani hapa mwovu huyo ambaye haipendi nchi yake? Kama yupo na aseme; kwani yeye nimemkosea. Nasubiri jibu.

RAIA: Hapana mtu, Buruto, hapana.

BURUTO: Basi sikumkosea mtu. Sikumfanyia lo lote Kaizari ambalo hamtaweza kumfanyia Buruto. Kisa cha kifo chake kimeandikwa Barazani; sifa zake hazikupunguzwa alipostahili; wala makosa yake hayakuzidishwa, yaliyomstahilisha kifo.

(*Aingia Antonio na wengine na maiti ya Kaizari*)

Huu mwili wake unakuja ukiombolezwa na Antonio; ambaye japo hakusaidia kumwua Kaizari, atafaidika kwa kifo hicho kwa kupata heshima katika dola. Kwani nani miongoni mwenu hatafaidika? Kwa kauli hii naondoka,—kama vile nilivyomwua rafiki yangu mpenzi kwa ajili ya Roma, ninao upanga ule ule kuutumia kwangu mwenyewe, itakapowapendeza wanachi wenzangu kutaka nife.

RAIA: Ishi, Buruto! Ishi, ishi!

RAIA 1: Mpelekeni kwa shangwe mpaka nyumbani kwake.

RAIA 2: Atengenezewe sanamu sawa na babu zake.

RAIA 3: Na afanywe Kaizari.

RAIA 4: Mema ya Kaizari yatatukuzwa kwa Buruto.

RAIA 1: Tumpeleke nyumbani kwa shangwe na vigelegele.

BURUTO: Wananchi wenzangu –

RAIA 2: Nyamazeni kimya, kelele! Buruto anasema.

RAIA 1: Kelele!

BURUTO: Wananchi wema, nacheni niondoke peke yangu; Kwa ajili yangu mimi bakini na Antonio: Yafanyieni heshima maiti ya Kaizari;

Na heshimuni hotuba atayotoa Antoni
Ya sifa za Kaizari, na ambayo Antonio
Karuhusiwa kutoa kwa ruhusa yetu sisi.
Kwa hiyo nawasihini asitoke mtu hapa
Ila mimi peke yangu hadi Antoni aseme.
(*Anaondoka*)

RAIA 1: Kaeni tumsikie Mariko Antonio.
RAIA 3: Na apande jukwaani; nasi tutamsikia.
Panda, Antonio bora.
ANTONIO: Kwa ajili ya Buruto nawashukuruni wote.
(*Anapanda jukwaa*)

RAIA 4: Amsemaje Buruto?
RAIA 3: Anasema kuwa yeye, kwa ajili ya Buruto,
Anatushukuru sote.
RAIA 4: Asirogwe akasema baya juu ya Buruto.
RAIA 1: Huyu Kaizari hasa alikuwa ni dhalimu.
RAIA 3: Hasa, hiyo ni dhahiri, nasi tumefadhilika,
Roma kuondokwa naye.
RAIA 2: Amani! tusikilize Antoni atalosema.
ANTONIO: Enyi Warumi wapole—
RAIA: Amani! Tumsikie.
ANTONIO: Rafiki zangu, Warumi, wananchi, nisikieni:
Mimi naja kumzika si kusifu Kaizari.
Maovu ya binadamu hudumu wakisha kufa;
Mara nyingi mema yao huzikwa pamoja nao;
Basi, iwe vivyo hivyo na kwa Kaizari pia.
Mheshimiwa Buruto kawaambieni kwamba
Kaizari alikuwa ni mtu mpenda cheo;
Kama hivyo ndivyo kweli lilikuwa kosa kubwa,
Na ambalo Kaizari kalilipia aghali.
Nipo hapa kwa idhini ya Buruto na wenziwe—
Maana Bwana Buruto ni mtu mheshimiwa,
Na wenziwe wote pia, wote ni waheshimiwa,
Nipate kuhutubia matanga ya Kaizari.

Alikuwa mwenzi wangu mwaminifu mwenye haki:
Ila Buruto asema kuwa alipenda cheo,
Na yeye Bwana Buruto ni mtu mheshimiwa.
Kaleta mateka wengi katika mji wa Roma,
Ambao fidia zao ziliyajaza maghala:
Kaizari kuyafanya hayo ni kupenda cheo?
Fukara walipolia, naye alilia nao:
Kupenda cheo kwataka moyo mgumu zaidi:
Bali Buruto asema kuwa alipenda cheo;
Na yeye Bwana Buruto ni mtu mheshimiwa.
Wote mlishuhudia siku ya Luperikali
Mara tatu nilimpa taji tukufu la enzi,
Kaizari mara tatu taji akalikataa:
Huko ni kupenda cheo?
Bali Buruto asema kuwa alipenda cheo;
Naye Buruto, hakika, ni mtu mheshimiwa.
Sisemi kuyakanusha aliyosema Buruto,
Ila mimi nipo hapa kusema niyajuayo.
Mlipata kumpenda, wala haikuwa bure:
Ni sababu gani, basi, sasa hamumlilii?
A, fahamu, umetoka, umekwenda kwa wanyama,
Na watu wamepoteza akili! Kunradhini;
Moyo wangu u kule na Kaizari jenezani,
Nami nitausubiri mpaka utakaporudi.
RAIA 1: Nadhani maneno yake ni maneno ya maana.
RAIA 2: Kama ukifikiria jambo hili kwa makini,
Kaizari kaonewa.
RAIA 3: Ameonewa, mabwana?
Nahofu asije mbaya zaidi badala yake.
RAIA 4: Mlishika manenoye? Alilikataa taji;
Na kwa hiyo ni hakika hakuwa mpenda cheo.
RAIA 1: Kama hivyo ndivyo wapo watakaolipa 'ghali.
RAIA 2: Lo, maskini! macho yamekuwa mekundu
Kama moto kwa kulia.

RAIA 3: Roma hako mtu bora kumzidi Antonio.
RAIA 4: Haya, msikilizeni, aanza tena kusema.
ANTONIO: Ni jana tu neno moja la Kaizari lingeza
Kuitikisa dunia: sasa amelala pale
Na hako hata fukara mmoja kumstahi.
A, mabwana, kama mimi ningependa kuitia
Mioyo na vichwa vyenu machafuko na ghadhabu,
Ningedhulumu Buruto, ningedhulumu Kasio,
Ambao, wote mwajua, ni watu waheshimiwa.
Hasha, sitawadhulumu; afadhali nichague
Kudhulumu marehemu, kujidhulumu mwenyewe,
Kuwadhulumuni nyinyi, kuliko kuwadhulumu
Watukufu kama hao. Ila hapa nina hati;
Ambayo imetiliwa muhuri wa Kaizari,
Ilikuwa sandukuni, nayo ni wosia wake;
Watu wangeusikia wosia wa Kaizari,
Ambao, kunradhini, sinuii kuusoma,
Wangekwenda wakabusu madonda ya Kaizari,
Na kuchovya vitambaa kwenye damuye takase;
Hata kuomba unywele wake uwe ukumbusho
Na wafapo wautaje katika wosia zao,
Kama hiba ya thamani kuvirithisha vizazi.
RAIA 4: Tuusikie wosia, tusomee, Antonio
WOTE: Wosia! Wosia! Soma wosia wa Kaizari.
ANTONIO: Enyi rafiki wapole, siyo vema niusome;
Si vizuri mfahamu jinsi alivyowapenda.
Ninyi si magogo; ninyi si mawe; bali ni watu:
Na kwa sababu ni watu, kama mkiusikia
Wosia wa Kaizari, utawasha nyoyo zenu,
Utawatia wazimu. Si vizuri mkijua
Kuwa mu warithi wake; kwani kama mkijua,
Lo, sijui matokeo yake yatakuwa nini!
RAIA 4: Soma wosia; lazima tuusikie, Antoni;
Natusomee wosia, wosia wa Kaizari.

ANTONIO: Tafadhali, subirini: fanyeni subira kwanza.
Nimefanya kosa kubwa kuwatajia wosia:
Nahofu nawakosea mabwana waheshimiwa
Walomwua Kaizari; nawakosea, nahofu.
RAIA 4: Walikuwa mahaini: mabwana waheshimiwa!
WOTE: Wosia! Wosia!
RAIA 2: Walikuwa majasusi, walikuwa wauaji;
Wosia, soma wosia!
ANTONIO: Basi mwanilazimisha niwasomee wosia?
Haya yazungushieni duara maiti yake
Ili niwaonyesheni mwandikaji wa wosia.
Je, niteremke chini? Nanyi mtaniruhusu?
WOTE: Shuka chini!
RAIA 2: Teremka!
RAIA 3: Utapatiwa ruhusa.
(*Antonio anateremeka chini*)
RAIA 4: Duara; fanyeni dwara.
RAIA 1: Simameni mbali na jeneza, mbali na maiti.
RAIA 2: Nafasi kwa Antonio, mtukufu Antonio.
ANTONIO: La, msinisonge hivyo, simamieni kwa mbali.
RAIA: Rudini nyuma! Nafasi haya sogeeni nyuma!
ANTONIO: Kama mnayo machozi jiandaeni kulia.
Nyote mwalijua joho hili; mimi nakumbuka
Siku ya kwanza kabisa Kaizari kulivaa;
Ilikuwa kiangazi, jioni, hemani mwake,
Siku alipowashinda Wanerivia vitani.
Tazameni, hapa ndipo Kasio alipochoma.
Tazameni pigo lake yule hasidi Kasika.
Na kipenziye Buruto, yeye alichoma hapa;
Na alipouchomoa upanga wake balaa,
Ona ilivyofuata damu yake Kaizari
Kama ikathibitishe kuwa ni kweli Buruto
Alichoma kikatili jinsi hiyo ama sivyo.
Kwani kama mjuavyo kipenzi cha Kaizari

Alikuwa ni Buruto. O, miungu, amueni,
Jinsi gani Kaizari alikuwa ampenda!
Hili ndilo lilikuwa pigo ovu la maovu;
Kwani Kaizari bora alipomwona kuchoma,
Utovu wa shukurani ulizizidi silaha
Ukamshinda; moyowe mkuu ukapasuka;
Na karibu na msingi wa sanamu yake Pompe,
Ambayo wakati wote ilibubujika damu,
Akaficha uso wake johoni akaanguka.
Lo, wananchi wenzangu, kianguko gani hicho!
Hapo, mimi, ninyi, sote jumla tulianguka,
Na uhaini mbaya ukitamba juu yetu.
Naona sasa mwalia; mnaonyesha huzuni:
Haya ni matone bora ya thamani kubwa sana.
Enyi, raia wapole, mnalia kwa kuona
Nguo tu za Kaizari wetu kutiwa madonda?
Tazameni hapa, basi, mwenyewe ni huyu hapa,
Kama mnavyomuona, kakatwa na mahaini.

RAIA 1: O, inasikitisha!
RAIA 2: O, mtukufu Kaizari!
RAIA 3: O, siku mbaya hii!
RAIA 4: O, mahaini, majasusi!
RAIA 1: O, ukatili gani huu!
RAIA 2: Tutalipiza kisasi!
WOTE: Kisasi! Haya! Saka! Choma! Moto! Ua! Fyeka!
Hata haini mmoja asibaki!
ANTONIO: Subirini, wananchi.
RAIA 1: Amani, msikieni mtukufu Antonio.
RAIA 2: Tutamsikia; tutamfata, na kufa naye.
ANTONIO: Rafiki wema, rafiki wapole, msiniache
Niwachochee maasi ya ghafula kama hayo.
Walotenda tendo hili ni watu waheshimiwa:
Ni manung'uniko gani ya siri waliyo nayo
Yalofanya wakatenda tendo ovu kama hili,

Ole wangu, sifahamu: lakini ni watukufu,
Na watu wenye busara, na wala hapana shaka
Watawajibu kwa hoja. Sikuja, rafiki zangu,
Kuwavuta mnifate. Mi si fundi wa kusema,
Kama Buruto alivyo; bali mtu kawaida,
Kama wote mjuavyo, nimpendaye mwenzangu;
Navyo ndivyo wajuavyo, walionipa ruhusa,
Nihutubu juu yake. Kwani sinazo akili
Maneno wala heshima, kitendo wala lafudhi,
Au nguvu za kusema kuchemsha watu damu.
Nasema mfululizo; nawaambieni mambo
Wenyewe muyajuayo. Nawaonyesha madonda
Yake Kaizari mwema, vinywa bubu, maskini,
Visivyoweza kusema, kuomba yanisemee:
Bali kama ningekuwa Buruto naye Antoni,
Mngekuwa na Antoni, ambaye angeliweza,
Kuchemsha roho zenu na kuingiza ulimi
Katika kila jeraha la Kaizari mkuu,
Ambao ungeyafanya hata na mawe ya Roma
Yacharuke na kuasi.

RAIA WOTE: Tutaasi!

RAIA 1: Tutaichoma nyumba ya Buruto.

RAIA 3: Haya basi! njooni, wasakeni mahaini!

ANTONIO: Hebu kwanza, wananchi; nisikieni niseme.

WOTE: Kimya! Sikieni Antonio, – Antonio bora.

ANTONIO: Mbona, rafiki, mwaenda kutenda msilojua:
Kaizari kafanyani hata alisitahili
Pendo lenu jinsi hiyo? Lo, hamna habari!
Basi, nitawambieni: mmesahau wosia,
Niliowatajieni.

WOTE: Ni kweli; wosia! Ngojeni tusikie wosia.

ANTONIO: Wosia ni huu, una muhuri wa Kaizari:
Anampa kila mtu, kila raia Mrumi,
Anamwachia ndarama sabini na tano zake.

RAIA 3: Mtukufu Kaizari! Tutalipa kifo chake.
RAIA 2: O, Kaizari maliki!
ANTONIO: N'sikieni kwa saburi.
WOTE: Amani, kimya!
ANTONIO: Tena kawaachieni barabara zake zote,
Bustani na mashamba yake mapya ya matunda
Yaliyo upande huu wa mto wa Tiberia;
Kawaachieni ninyi na wana wenu milele:
Anasa za kila mtu, mwende mjiburudishe.
Huyu, basi, alikuwa Kaizari mhisani!
Mwingineo kama yeye atakuja siku gani?
RAIA 1: Haji tena asilani! Njoni, twendeni, twendeni!
Tutauchoma mwiliwe pahali patakatifu
Na vimuli tuchomee nyumba zao mahaini.
Yachukueni maiti.
RAIA 2: Tafuteni moto!
RAIA 3: Vunjeni mabao!
RAIA 4: Vunjeni mabao, madirisha, cho chote!

(*Raia wanatoka na maiti*)

ANTONIO: Balaa, umeshazuka, sasa fanya upendavyo!

(*Anaingia Mtumishi*)

Je, kuna habari gani?
MTUMISHI: Bwana, Ottavio kesha kufika mjini Roma.
ANTONIO: Yuko wapi?
MTUMISHI: Nyumbani kwa Kaizari, yu pamoja na Lepido.
ANTONIO: Nami nitakwenda huko sasa hivi kumfata:
Kaja wakati mzuri. Bahati inafurahi
Na katika hali hii 'tatupatia cho chote.
MTUMISHI: Nilimsikia akisema ya kuwa Buruto
Na Kasio wamekimbia wakapita katika
Milango ya Roma kama wenye kuwa na wazimu.
ANTONIO: Yumkini wamepata habari za wananchi,
Nilivyowachemsha. Nipeleke kwa Ottavio.

Onyesho la III: Barabarani

(*Anaingia Sinna mshairi*)

SINNA: Niliota leo kuwa nilikuwa karamuni
Pamoja na Kaizari; tena nina kisirani.
Kutoka na kutembeatembea sinayo nia,
Walakini kuna kitu kiniongozacho njia.

(*Wanaingia Raia*)

RAIA 1: Jina lako nani?
RAIA 2: Unakwenda wapi?
RAIA 3: Unakaa wapi?
RAIA 4: Umeoa, ama sivyo?
RAIA 2: Mjibu kila mmoja kwa wazi.
RAIA 1: Naam, tena kwa kifupi.
RAIA 4: Naam, tena kwa busara.
RAIA 3: Na itakufaa ujibu kwa ukweli.
SINNA: Jina langu mimi nani? Tena ninakwenda wapi?
Masikani yangu wapi? Nimeoa ama sivyo?
Basi, sasa kumjibu kila mtu wazi wazi,
Kwa kifupi, kwa busara, na ukweli ninasema:
Kwa busara sijaoa.
RAIA 2: Yaani unatwambia watu wote walooa
Ni wajinga maluuni: ngoja utanitambua.
Endelea, waziwazi.
SINNA: Waziwazi, nafuata mazishi ya Kaizari.
RAIA 1: Kama rafiki au adui?
SINNA: Nakwenda kama rafiki.
RAIA 2: Hilo umejibu wazi.
RAIA 3: Maskani, —kwa kifupi.
SINNA: Kwa kifupi ninaishi karibu na Bunge Kuu,
RAIA 3: Jina lako, bwana, kwa ukweli.
SINNA: Kwa ukweli jina langu mimi ninaitwa Sinna
RAIA 1: Mrarueni vipande; ni haini msaliti.
SINNA: Mimi Sinna mshairi, Sinna mshairi, mie.

RAIA 4: Mrarueni kwa hayo mashairiye mabaya.
SINNA: Mimi siye yule Sinna msaliti.
RAIA 4: Haidhuru, asilani, naye jinale ni Sinna.
Rarueni jina lake kwenye moyo wake afe.
RAIA 3: Mrarueni, mrarueni! Haya, vimuli ho! vimuli vya moto:
Kwa Buruto, kwa Kasio; choma kila kitu: wengine
nyumbani kwa Desio, na wengine kwa Kasika; wengine
kwa Ligario: haya twende!

(*Wanaondoka*)

IV

Onyesho la I: Nyumbani, mjini Roma

(*Antonio, Ottavio, na Lepido wamekaa mezani*)

ANTONIO: Kwa hiyo tumekubali, hawa wote watakufa;
Majina yao tayari, yameshatiwa alama.
OTTAVIO: Na nduguyo atakufa; unakubali, Lepido?
LEPIDO: Nakubali –
OTTAVIO: Mtie alama, Antonio.
LEPIDO: Kwa sharti hili moja, kwamba Pubulio pia,
Mpwa wako, Antonio, naye pia hataishi.
ANTONIO: Hataishi; angalia, kwa doa namlaani.
Lakini, Lepido, nenda nyumbani kwa Kaizari;
Kalete wosia hapa ili tuone namna
Ya kupunguza malipo mengineyo ya urithi.
LEPIDO: Nitawakuteni hapa?
OTTAVIO: Usipotukuta hapa,' tatukuta Barazani.

(*Lepido anatoka*)

ANTONIO: Huyu ni mtu dhalili asostahili kitu,
Afaaye kutumwa tu: naye itafaa kweli,
Dola itapogawanywa katika sehemu tatu,
Awe kati ya watatu watakaoigawana?
OTTAVIO: Ndivyo ulivyomwazia, ukamtaka shauri.
Wakati wa kuamua, nani watakaokufa,
Katika orodha yetu ya wenye kuhukumiwa.
ANTONIO: Ottavio, nimeona siku nyingi kukuzidi:
Tungampa mtu huyu utukufu wote huu,
Ili kujipunguzia mzigo wa malawama;
Taubeba kama punda anavyobeba dhahabu,
Kilalama na kutoka jasho kwa uzito wake,

Kiongozwa na kuswagwa vile tutavyomwonyesha;
Na mara afikishapo amana tupapendapo,
Tutamtua mzigo wake na kumwachilia
Sawa na punda mtupu, atikise masikio,
Ajiendee mbugani, akale majani yake.

OTTAVIO: Timiza utashi wako; lakini yu askari
Jarabati na shujaa.

ANTONIO: Punda wangu vile vile, Ottavio, yuko vivyo;
Basi kwa ajili hiyo namgawia chakula:
Kiumbe ambaye mimi namfunza kupigana,
Kuzunguka, kusimama, kukimbia mfulizo,
Mwendo wa viungo vyake huitii nia yangu.
Na kwa upande mwingine Lepido ndivyo alivyo;
Ili apate kuenda hana budi afundishwe,
Azoezwe na atumwe; ni kiumbe hohehahe,
Aishiye kwa makombo, masalia na kuiga,
Mambo yalokwisha chuja na kuachwa na wengine,
Kwake huwa fani mpya. Haifai kumtaja,
Ila kama ni chombo tu. Basi sasa, Ottavio,
Sikia mambo makubwa:—Buruto naye Kasio
Wanaandika majeshi: ni lazima tupigane.
Kwa hiyo na tuungane, tupate na marafiki,
Na uwezo wetu wote tuutumie vizuri;
Na pasipo kuchelewa, twende zetu tukutane,
Ili tukatafakari jinsi ya kutambulisha
Yale yaliyofichika, na jinsi ya kukabili
Hatari za wazi wazi.

OTTAVIO: Haya na tufanye hivyo: kwani tuko hatarini,
Na wanaotuchekea, sina shaka asilani,
Wengine wana maovu mengi mioyoni mwao.

Onyesho la II: Kambini, karibu na Sardisi. Nje ya hema la Buruto

(*Ngoma: wanaingia Buruto, Lusilio, Titinio, na Askari Pindaro anawalaki. Lukio yuko mbali kidogo*)

BURUTO: Simama, ho!
LUSILIO: Toa neno, ho! na usimame.
BURUTO: Kuna nini, Lusilio? Kasio yuko karibu?
LUSILIO: Yu karibu, na Pindaro kakuletea salamu
Kutoka kwa bwana wake.
(*Pindaro anampa Buruto barua*)
BURUTO: Kanisalimu vizuri.—Bali Bwanao, Pindaro,
Ama kwa kubadilika, ama sivyo, kwa sababu
Ya maofisa wabaya kanipa sababu tosha
Kunifanya nitamani yale yaliyotendeka
Yawe hayakutendeka: bali kama yu karibu
Nitamwomba aneleze.
PINDARO: Sina shaka mtukufu bwanangu utamkuta
Yu vile vile, mstahi, na mwenye heshima nyingi.
BURUTO: Simtilii mashaka. Tafadhali, Lusilio,
Nataka unijulishe ulivyopokewa naye.
LUSILIO: Kwa jamala, na heshima inayotosha kabisa;
Bali pasi na dalili zo zote za mazoea,
Na bila mazungumzo ya wazi na kirafiki,
Kama alivyozoea kufanya hapo zamani.
BURUTO: Umeeleza rafiki aliyekuwa na moyo
Unaopooza sasa: sikuzote, Lusilio,
Kumbuka kuwa mapenzi yakianza kuugua
Na kuoza hutumia upole wa takalifu;
Imani iliyo safi na wazi haina hila:
Walakini wanafiki, wana moyo wa farasi,
Ambao huuonyesha moyo wao kwa makeke,
Ila mara wapatapo uchungu wa vichocheo
Basi huangukwa shingo kama vihongwe waongo

Kwa huko kujaribiwa. Jeshi lake linakuja?
LUSILIO: Wataka wapige kambi Sardisi kwa usiku.
Walo wengi, ambao ni askari wa farasi,
Wamekuja na Kasio.
(*Gwaride ndani*)
BURUTO: Sikia! Kafika: – nenda taratibu umlaki.
(*Aingia Kasio na Askari*)
KASIO: Simama, ho!
BURUTO: Simama, ho! Toa neno upite.
ASKARI 1: Simama!
ASKARI 2: Simama!
ASKARI 3: Simama!
KASIO: Ndugu mtukufu, umenionea.
BURUTO: Nihukumuni, miungu! Naonea maadui?
Kama sivyo, nawezaje kumwonea ndugu yangu?
KASIO: Buruto, utuvu wako huu huficha maovu,
Na unapoutenda –
BURUTO: Kasio, tafadhali; –
Yaseme maudhi yako taratibu, – nakujua.
Haifai kugombana hapa katika hadhara,
Mbele ya majeshi yetu, ambayo si jambo zuri
Yaone ugomvi ila mapenzi baina yetu.
Yaamrishe yatoke; halafu hemani kwangu,
Kasio, utaeleza zaidi maudhi yako,
Nami ’takusikiliza.
KASIO: Pindaro, kawaambie maamiri jeshi wetu
Wayapeleke majeshi mbali kidogo na hapa.
BURUTO: Lusilio, nawe nenda ukafanye vivyo hivyo;
Wala asije ye yote kule kwenye hema letu
Mpaka twishe mkutano. Lusilio, Titinio,
Lindeni mlango wetu.
(*Wanatoka*)

Onyesho la III: Hemani mwa Buruto

(*Aingia Buruto na Kasio*)

KASIO: Kwamba umenionea sababu yake ni hii:
Umemsuta Pindaro Pella na kumfedhehi.
Kwa kuwa katwaa rushwa hapa kwa Wasardia;
Na nilipokwandikia kumwombea msamaha,
Kwa sababu namjua, ulipuzilia mbali.
BURUTO: Wewe ulijionea kwa kuweza kuandika,
Penye jambo kama hilo.
KASIO: Kwa wakati kama huu, si vizuri kila kosa,
Ijapokuwa ni dogo, liwe likishutumiwa.
BURUTO: Subiri nikuambie, Kasio, na wewe pia
Una kosa kubwa sana kwa kupenda milungula;
Kwa kuuza na kunadi vyeo vyako kwa dhahabu,
Kwa watu wasiofaa.
KASIO: Mi napenda milungula!
Watambua ni Buruto ambaye wasema hivi,
La sivyo, nakuapia, ya kuwa kauli hii,
Kwa hakika ingekuwa kauli yako ya mwisho.
BURUTO: Kasio kauachia uovu wa rushwa huu,
Kwa hiyo adhabu yake inayaficha makali.
KASIO: Adhabu!
BURUTO: Kumbuka Machi, kumbuka, siku ya kati ya Machi.
Kaizari mtukufu, alichofia si haki?
Kuna hayawani gani alogusa mwili wake
Na kuuchoma upanga kama sababu si haki?
Na sasa mmoja wetu tulomwua mtu bora
Wa dunia kwa sababu alilinda wanyang'anyi,
Sasa tuvitie doa vidole vyetu wenyewe,
Kwa virushwa na kuuza vyeo vyetu kwa uchafu,
Unopatikana hivyo? Ni heri nikawa mbwa,
Na kuubwekea mwezi kuliko kuwa Mrumi

Wa aina kama hiyo.
KASIO: Basi, usinibwekee; siwezi kuvumilia:
Wajisahau mwenyewe kunibanabana hivi;
Mimi askari mimi, wa siku nyingi zaidi,
Mwenye uwezo zaidi wa kutoa masharti.
BURUTO: Wapi; huwezi, Kasio.
KASIO: Naweza.
BURUTO: Mimi nasema huwezi.
KASIO: Usiniudhi zaidi au nitajisahau;
Fikiri salama yako, usiniudhi zaidi.
BURUTO: Ondoka, hayawani we!
KASIO: Inawezekana kweli?
BURUTO: Nisikie, nitasema.
Ni lazima nizijali hasira zako za ovyo?
Nihofu mwenda wazimu anapokodoa macho?
KASIO: Enyi miungu, miungu, nihimili yote haya?
BURUTO: Yote haya na zaidi. Jisumbue kwa hasira
Mpaka moyo wako wenye majivuno upasuke;
Kazionyeshe hasira zako kwa watumwa wako;
Kawafanye waja wako wateteme. Basi, nami
Nistuke? Nami pia nikujali? Nisimame
Na kupigishwa magoti na kani zako za ovyo?
Naapa, utaimeza sumu ya ghadhabu yako
Japo ikikupasua; kwani mimi tangu leo
Takutumia kwa nia ya kunifurahisha tu,
Naam, na kunichekesha, utakapokasirika.
KASIO: Imefika kima hiki?
BURUTO: Unasema kuwa wewe eti askari bora:
Hebu thibitisha, basi: timiza kujigambakwo,
Nitafurahika sana: mimi kwa upande wangu,
Nitafurahi kuiga kwa watu walio bora.
KASIO: Wanionea Buruto: ko kote wanionea.
Nilisema askari wa siku nyingi zaidi,
Sikusema kuwa bora: nilisema mimi bora?

BURUTO: Japo kama ulisema, wala nisingelijali.
KASIO: Wala Kaizari hai asingethubutu kamwe
Kuniudhi kama hivi.
BURUTO: Tulizana, tulizana, wewe usingethubutu
Kumchokozaye hivi.
KASIO: Mimi nisingethubutu!
BURUTO: Kamwe usingethubutu!
KASIO: Mimi nisingethubutu kuchokoza Kaizari?
BURUTO: Kwa kuhofia maisha yako usingethubutu
KASIO: Usitegemee mno mapenzi yangu kwakowe;
Naweza nikalifanya jambo la kunijutisha.
BURUTO: Umekwisha kulifanya jambo la kukujutisha.
Vitisho vyako, Kasio, ni vya upuzi kabisa,
Kwani ninayo silaha ya kutosha – moyo safi –
Na nisiowaheshimu hunipita kama vumbi.
Niliagiza dhahabu kiasi ukaninyima:
Kwani siwezi kutoza fedha kwa njia haramu:
Kweli heri niufue moyo wangu uwe fedha,
Kuliko kuikamua mikono ya wakulima
Vitaka vyao vya ovyo kwa njia iliyo mbaya.
Niliagiza dhahabu nilipe majeshi yangu,
Na wewe ukaninyima: uliponinyima hivyo,
Ulitenda ki-Kasio? Mimi Kayusi Kasio
Ningelimjibu hivyo? Kweli Mariko Buruto
Atapokuwa mchoyo kuwahini rafikize
Takataka kama hizo, jiandaeni, miungu,
Kwazo radi zenu zote, kumpasua vipande.
KASIO: Sikukunyima, Buruto.
BURUTO: Kasio, ulininyima.
KASIO: Nasema sikukunyima: aloleta jibu langu
Alikuwa mpumbavu: Buruto kan'kata moyo:
Makosa yake rafiki, rafiki huyahimili;
Ila Buruto hukuza yangu kupita yalivyo.
BURUTO: Sifanyi hivyo ila tu unapoyatenda kwangu.

KASIO: Hunipendi.
BURUTO: Sipendi makosa yako.
KASIO: Kweli jicho la rafiki kamwe lisingeyaona
Makosa namna hiyo.
BURUTO: Jicho lake mnafiki kamwe lisingeyaona
Hata kama yangekuwa makubwa kama Olimpo.
KASIO: Njoo, Antonio, njoo, na kijana Ottavio,
Malizieni kisasi kwa Kasio peke yake,
Maana kweli Kasio kesha choshwa na dunia;
Achukiwa na mwenzie yeye anayempenda;
Akaripwa na nduguye; anagombezwa kitumwa;
Hitilafu zangu zote zimechunguliwa vema
Na kwandikwa kitabuni, zisomwe, zikaririwe,
Nitupiwezo usoni. O, natamani kulia
Maisha yangu machoni; upanga wangu ni huu,
Na kifua changu hiki, wazi; ndani kina moyo
Ambao ni bora kupita mashimo ya Puluto;
Ambao una thamani inayozidi dhahabu:
Kama wewe ni Mrumi, basi, uchukue sasa;
Nilokunyima dhahabu nakupao moyo wangu:
Choma ulivyouchoma moyo wake Kaizari;
Kwani natambua kuwa ulipomchukiato
Ulimpenda zaidi kuliko ulivyopata
Ukampenda Kasio.
BURUTO: Futika upanga wako: kasirika upendapo,
Kani yako iridhike; fanya kama upendavyo,
Yote kwangu ni kicheko; Kasio, 'mefungwa nira
Pamwe na mwana kondoo, ambaye ana ghadhabu,
Jiwe lilivyo na moto; kama jiwe likigongwa,
Mara cheche hutokea, mara hutoweka tena.
KASIO: Kasio amesha kuwa kichekesho cha Buruto,
Kwa kuwa kusumbuliwa na huzuni na ghadhabu?
BURUTO: Na mimi niliposema nilikuwa na ghadhabu.
KASIO: Wakiri kiasi hicho? Ulete mkono wako.

BURUTO: Hata moyo wangu pia.
KASIO: O, Buruto –
BURUTO: Nini?
KASIO: Hivi huna mapenzi ya kunistahimilia
Kilema cha ushupavu alichonipa mamangu
Kufanya nighafilike?
BURUTO: Naam, na tangu sasa, Kasio, saa yo yote
Ukimghadhibikia Buruto wako tasema,
Ya kuwa ni mama yako ndiye anakugombeza,
Na kukwacha vivyo hivyo.
MSHAIRI: (*Ndani*) Nachie niende ndani nione majemadari;
Wana jambo kati yao si vema wakiwa peke.
LUSILIO: (*Ndani*) Huwezi kuwafikia.
MSHAIRI: (*Ndani*) Sipingwi ila kwa kifo.
(*Aingia Mshairi akifuatwa na Lusilio, Titinio na Lukio*)
KASIO: Kuna nini?
MSHAIRI: Majemadari ninyi;
Hamna haya?
Mambo gani haya?
Pendaneni kirafiki,
Inavyostahiki
Kwa wawili kama ninyi;
Kwani nina hakika
Nimeona mingi miaka
Zaidi kuliko ninyi.
KASIO: Ha, ha! Sikia utenzi mbaya wa mshenzi huyu!
BURUTO: Nenda zako, wee; fidhuli wee, ondoka hapa!
KASIO: Mstahimili Buruto; ndiyo desturi yake.
BURUTO: Nitamstahimili achaguapo wakati;
Vinahusiana nini vita na wenye utenzi
Wapumbavu kama hawa? Haya, ondoka hapa, we!
KASIO: Haya, haya, nenda zako!
(*Mshairi anaondoka*)
BURUTO: Lusilio, Titinio, haya kawaambieni

Maamiri wa majeshi kuwa wajitayarishe
Kupumzisha majeshi yao usiku wa leo.
KASIO: Mkisha rudini kwetu mara pamwe na Messala.
(*Lusilio na Titinio wanaondoka*)
BURUTO: Lukio, tafadhali, nipe bakuli la mvinyo!
KASIO: Sikudhani unaweza kuudhika kama vile.
BURUTO: O, Kasio, nalemewa na maafa mengi mno.
KASIO: Kanunizo hazifai ikiwa unakubali
Kulemewa na maafa yasokuwa na maana.
BURUTO: Hapana anizidiye kuvumilia maafa –
Poshia amefariki.
KASIO: A! Poshia!
BURUTO: Amekufa.
KASIO: Niliepukaje kufa nilipokuudhi vile?
Msiba uso kiasi! Oo, majuto mazito!
Kafa kwa ugonjwa gani?
BURUTO: Kushindwa kuvumilia kukosa kuwapo kwangu,
Na huzuni ya kwambiwa kuwa Mariko Antoni
Na kijana Ottavio wamepata nguvu sana;—
Kwani habari za kifo zilikuja nazo hizo;—
Naye ’kakata tamaa; basi watumishi wake
Walipokuwa hawapo yeye akameza moto.
KASIO: Na ndivyo alivyokufa?
BURUTO: Naam.
KASIO: O, miungu wa milele!
(*Lukio anarudi na mvinyo na mwenge*)
BURUTO: Basi, simtaje tena. Nipe kombe la mvinyo.
(*Anakunywa*)
Humu, Kasio, nazika utovu wote wa wema.
KASIO: Moyo wangu una kiu cha azima bora hiyo.
Jaza mvinyo, Lukio, hadi chombo kifurike;
Sina kikomo cha kunywa kwa kipenzi cha Buruto.
(*Anakunywa*)
(*Lukio anatoka*)

(*Titinio anarudi pamoja na Messala*)

BURUTO: Karibuni, Titinio! Karibu, Messala mwema.
Sasa, basi, na tukae karibu na mwenge huu,
Tuweze kufikiria mambo tunayohitaji.
KASIO: Poshia, umeondoka
BURUTO: 'Simtaje, nakusihi.
Messala, nimepokea barua zinazosema
Bwanamdogo Ottavio na Antoni watujia
Wana jeshi kubwa sana waelekea Filippi.
MESSALA: Nami ninazo barua za namna hiyo hiyo.
BURUTO: Na habari gani tena?
MESSALA: Kwamba kwa kubatilisha, Ottavio, Antonio,
Na Lepido wameua maseneta mia moja.
BURUTO: Kwa hapo barua zetu zinahitilafiana;
Zangu zataja sabini maseneta walokufa
Kwa kubatilishwa huko, mmoja wao Sisero.
KASIO: Sisero mmoja wao?
MESSALA: Naam, Sisero kafa, kwa sheria hiyo hiyo.
Ulipokea barua zako toka kwa mkeo,
Bwana wangu?
BURUTO: La, Messala.
MESSALA: Wala habari yo yote katika barua zako,
Ambayo inamhusu?
BURUTO: La, Messala.
MESSALA: Hiyo, basi, ni ajabu.
BURUTO: Kwa nini umeuliza? Umesikia habari
Yo yote imhusuyo katika barua zako?
MESSALA: La, bwana wangu.
BURUTO: Ukiwa Mrumi hasa, basi nambie ukweli.
MESSALA: Basi, pokea ki-Rumi ukweli nitokwambia:
Kwa kweli amefariki, na kwa njia ya ajabu.
BURUTO: Basi, kwa heri, Poshia. Lazima tufe, Messala:
Kwa kujua kuwa iko siku moja atakufa
Naweza kuvumilia hiki kifo chake sasa.

MESSALA: Hivyo ndivyo ipasavyo wakubwa kuvumilia
Misiba yao mikubwa.
KASIO: Na mimi pia ninao ufundi huu kamawe,
Bali nisingeliweza kustahimili hivyo.
BURUTO: Haya, na tuwe kazini, sisi ambao tu hai.
Waonaje tukienda Filippi kwa hivi sasa?
KASIO: Mimi nafikiri kuwa haitakuwa vizuri.
BURUTO: Sababu yako ni nini?
KASIO: Sababu yangu ni hii:
Ni jambo bora zaidi adui atufuate:
Yeye akitufuata, atajipunguza nguvu,
Atachosha majeshiye, ajipatie hasara.
Bali sisi kwa kutua tutapumzika sana,
Tutaweza kujilinda na tutakuwa wepesi.
BURUTO: Hoja nzuri ni lazima zizipishe hoja bora.
Watu kati ya Filippi na hapa tulipo sasa
Ni watu watupendao kama kwa kushurutishwa;
Maana wametusunza msaada wa askari:
Adui awapitie, atawamega baadhi,
Ajiongezee nguvu aje ameburudika,
Ameongezeka sana, na pia katiwa moyo.
Bali tutamzuia kupata nafuu hiyo,
Kama sisi tukienda kumkabili Filippi,
Na kufanya watu hawa wawe wako nyuma yetu.
KASIO: Nisikie, ndugu mwema –
BURUTO: Tafadhali – huna budi utambue pia kwamba
Jeshi letu limejaa, nia yetu imeiva:
Na adui kila siku azidi kuongezeka;
Kwa kuwa tu kileleni tutaanza kwenda chini.
Majambo ya binadamu yana kujaa na kupwa,
Yakidakwa yamejaa huongoza ushindini;
Yakipuuzwa, safari yote ya maisha yao
Haiachi maji mafu, na hujaa madhilifu.
Sisi sasa twaelea katika maji makuu;

Twapaswa kuyatumia yangali yakitufaa,
Ama sivyo tutakosa yote tuloazimia.
KASIO: Basi, ili kutimiza mapenziyo, tangulia;
Nasi pia tutakuja na kuwakuta Filippi.
BURUTO: Ni usiku wa manane na tungali tukisema,
Tabia haina budi kuyatii ya faradhi.
Na sisi na tuyatii kwa usingizi kidogo.
Bado kuna la kusema?
KASIO: Hapana jambo. Kwa heri.
Na tujidamke kesho na kuanza kusafiri.
BURUTO: Lukio! (*Lukio anaingia*) Nguo yangu.
(*Lukio anatoka.*)
Kwaheri, Messala mwema; buriani, Titinio:
Na Mtukufu Kasio mtukufu, buriani,
Na ukalale salama.
KASIO: O, mpenzi ndugu yangu, huu leo ulikuwa
Mwanzo mbaya wa usiku: utengano kama huu
Usije kurudi tena baina ya nyoyo zetu!
Usije tena, Buruto.
BURUTO: Mambo yote ni salama.
KASIO: Buriani, bwana wangu.
BURUTO: Buriani, ndugu mwema.
TITINIO na MESSALA: Kwa heri, Bwana Buruto.
BURUTO: Kwa heri, kila mmoja.
(*Kasio, Titinio na Messala wanatoka*)
(*Lukio anarudi na nguo*)
Nipe hiyo nguo yangu. Chombo chako kiko wapi?
LUKIO: Ki hapa ndani ya hema.
BURUTO: Wasema kwa kusinzia? Sikulaumu, kijana;
Umelinda saa nyingi. Kamwite Kilaudio,
Na ba'dhi ya watu wangu; na waje hemani kwangu
Walale juu ya mito.
LUKIO: Varro na Kilaudio!
(*Wanaingia Varro na Kilaudio*)

VARRO: Bwana wangu ameita?
BURUTO: Tafadhali jinyosheni hemani kwangu,mabwana,
Na mjaribu kulala. Huenda niwaamshe
Baadaye niwatume kwa ndugu yangu Kasio.
VARRO: Mapenziyo yatimie; sisi tutakaa macho
Kusubiri utashiwo.
BURUTO: Sikubali msubiri: laleni, mabwana wema.
Pengine yawezekana nikabadili mawazo;
Ona, Lukio, kitabu nilichonikitafuta:
Kilikuwa mfukoni.
(*Varro na Kilaudio wanajinyoosha*)
LUKIO: Nilikuwa na hakika bwana wangu hakunipa.
BURUTO: Kunradhi, kijana mwema, ninaghafilika sana.
Huwezi ukawa macho japo kwa muda mfupi,
Na kupiga wimbo moja au nyimbo mbili hivi?
LUKIO: Ninaweza, bwana wangu, kama itakupendeza
BURUTO: Itanipendeza, baba:
Ninakusumbua mno, lakini unakubali.
LUKIO: Ni wajibu wangu, bwana.
BURUTO: Sina haki kukudai wajibu wako kuzidi
Uwezo wako; najua kuwa damu ya ujana
Hutaka sana ipate saa ya kupumzika.
LUKIO: Nimelala, bwana wangu.
BURUTO: Ni vizuri ulilala; na utalala zaidi.
Sitakukawiza mno: kama nitaishi bado
Nitakufanyia wema.
(*Muziki na wimbo: mwishoni Lukio anasinzia na kulala*)
Huu wimbo wa kulaza: – O, usingizi mfisha,
Kwa rungulo zito sana umempiga mwanangu
Akupigiaye nyimbo? Kijana mwema, kwa heri.
Kama nikikuamsha takuwa nakukosea:
Na kama ukiinama utavunja chombo chako;
Basi, nitakiondoa; kwa heri, kijana mwema.
Hebu nione; nadhani ukurasa umekunjwa

Pale nilipoachia. Nafikiri ndipo hapa.
(*Mzuka wa Kaizari unaingia*)
Mwenge huu unawaka vibaya! Ha! Huyu nani?
Nadhani ni udhaifu wa macho yangu mwenyewe,
Unaozusha dubwana baya hili la mzuka.
Lanijongea karibu. Wewe, u kitu cho chote?
U muungu, malaika, au wewe ni shetani,
Unigandishaye damu na kusisimua nywele?
Nambie, wewe ni nani?
MZUKA: Pepo mbaya wa Buruto.
BURUTO: Waletwa na jambo gani?
MZUKA: Kukuambia ya kuwa utaniona Filippi.
BURUTO: Vema; kwa hiyo tuseme kuwa nitakwona tena?
MZUKA: Naam, utaniona Filippi.
BURUTO: Vema, basi, nitakuona Filippi.
(*Mzuka unatoka*)
Sasa nimepata moyo na wewe unatoweka:
Pepo mwovu, ningependa tuzungumze zaidi.
Mtoto Lukio! Varro! Kilaudio! Mabwana,
Amkeni! Kilaudio!
LUKIO: Nyuzi mbaya, bwana wangu.
BURUTO: Adhani kuwa angali anapiga chombo chake.
Lukio, amka!
LUKIO: Bwana wangu.
BURUTO: Je, Lukio, uliota, kupiga kelele hivyo?
LUKIO: Bwana wangu, sifahamu kuwa 'mepiga kelele.
BURUTO: Ndiyo, umepiga sana: vipi, uliona kitu?
LUKIO: Sikwona cho chote, bwana.
BURUTO: Lala tena, Lukio Kilaudio! (*kwa Varro*) We, amka.
VARRO: Bwana wangu?
KILAUDIO: Bwana wangu?
BURUTO: Mabwana, 'lipigiani kelele usingizini?
VARRO na KILAUDIO: Tulipiga kweli bwana?
BURUTO: Naam: mliona kitu?

VARRO: La, bwana, sikwona kitu.
KILAUDIO: Wala mimi, bwana wangu.
BURUTO: Nendeni mkamsalimu ndugu yangu, Kasio;
Mwambieni aondoke na majeshiye mapema,
Na sisi tutafuata.
VARRO na KILAUDIO: Itafanywa, bwana wangu.
(*Wanaondoka*)

V

Onyesho la I: Mbugani - Filippi

(*Wanaingia Ottavio, Antonio, na Jeshi lao*)

OTTAVIO: Sasa, matumai yetu yametimu, Antonio:
Ulisema maadui hawashuki tambarare;
Watabaki vilimani na kwenye nyanda za juu:
Lakini sivyo ilivyo; majeshi yao yaaja;
Ili kutushambulia kwa papa hapa Filippi;
Wanaitika kabla sisi hatujawaita.

ANTONIO: Wapi! Nawajua sana, tena najua kwa nini
Wao wamefanya hivyo. Wangependelea sana
Kwenda sehemu nyingine; bali wametelemka,
Wajidai kutishia, kufanya tuwadhanie
Kuwa mashujaa sana; na kumbe sivyo ilivyo.

(*Aingia Tarishi*)

TARISHI: E, ninyi majemadari, jiandaeni kwa vita:
Maadui wanakuja kwa fani za kishujaa;
Alama yao ya vita inapepea angani;
Lazima lifanywe jambo hima bila kuchelewa.

ANTONIO: Ottavio, yaongoze majeshiyo pole pole,
Kushoto ya tambarare.

OTTAVIO: Mimi 'takuwa kulia: wewe na uwe kushoto.

ANTONIO: Kwa nini unanipinga saa ya hatari hii?

OTTAVIO: Mimi sikupingi wewe, bali ndivyo tavyofanya.

(*Mwendo wa askari*)

(*Ngoma. Wanaingia Buruto, Kasio, na jeshi lao*)

BURUTO: Wasimama, watapenda mashauriano kwanza.

KASIO: Kita hapa, Titinio; twaenda kuzungumza.

OTTAVIO: Je, Mariko Antonio, tuamrishe pigano?

ANTONIO: La, Kaizari, tutaitika wakishambulia.
Na twende, majemadari wapenda mazungumzo.
OTTAVIO: Msifanye jambo mpaka sisi tutoe ishara.
BURUTO: Maneno kabla ya vita? Hivyo ndivyo, wananchi?
OTTAVIO: Si kwamba tu kama nyinyi, wapendelea maneno.
BURUTO: Neno jema, Ottavio, linazidi pigo baya.
ANTONIO: Wewe, Buruto, katika mapigo yako mabaya,
Hubwata maneno mema. Kumbuka ulivyochoma
Moyo wake Kaizari, huku wapiga kelele,
'Aishi dumdaima! Atukuzwe Kaizari!'
KASIO: Antoni, mapigo yako bado hayajulikani;
Lakini maneno yako ni matamu, utadhani
Yamewaibia nyuki wa Hibla mizingani,
Na kuwaacha watupu bila kuwa na asali.
ANTONIO: Lakini hawakuachwa watupu bila makali.
BURUTO: Naam, na bila sauti; kwani umewaibia
Na mvumo, Antonio; hivyo kwako ni busara
Utishie kwa kuvuma, na halafu ukauma.
ANTONIO: Enyie mahayawani, nyi hamkufanya hivyo,
Mapanga yenu maovu yalipojikatakata
Mbavuni mwa Kaizari: lakini kama manyani
Mlitoa meno nje mkacheka kama mbwa
Mkasujudu kitumwa, mkambusu miguu;
Huku Kasika laana, kama mbwa, mgongoni,
Akamchoma shingoni, Kaizari mtukufu.
O, walaghai wakuu!
KASIO: Walaghai! Haya sasa, Buruto ujishukuru.
Kasio angesikiwa, hakika ulimi huu
Leo usingeliweza kutoa fidhuli hii.
OTTAVIO: Haya, na tuanze kazi: kama kubishana huku
Kwafanya tutoke jasho, basi kukuthibitisha
Lazima kutoe damu. Ona, natoa upanga,
Kuwapiga mahaini; unafikiri ni lini
Nitaufutika tena? Hautafutikwa kamwe,

Mpaka majeraha yote thelathini na matatu
Ya Kaizari yalipwe; au mpaka auawe
Kaizari mwinginewe, kwa panga za mahaini.

BURUTO: Kaizari, hutakufa kwa panga za mahaini
Isipokuwa mwenyewe uwe umekuja nao.

OTTAVIO: Nami pia hivyo ndivyo ninavyotumainia;
Sikuzawa ili nife kwa upanga wa Buruto.

BURUTO: O, kama ungelikuwa kito cha ukoo wenu,
Hungekufa, we kijana, kifo kizuri zaidi.

KASIO: Kitoto cha shule tu, kasirani, kipumbavu,
Kisichoustahili utukufu kama huo,
Pamoja na mchezaji na mtafuta anasa!

ANTONIO: Yu Kasio yule yule!

OTTAVIO: Njoo, Antonio, twende!
Kinywani mwenu, twatema shari, enyi mahaini:
Mkiweza kupigana leo njoni uwanjani;
La, hamwezi, basi hapo mtakapopata moyo.
(*Ottavio, Antonio na Jeshi lao wanaondoka*)

KASIO: Na, sasa, vuma upepo, vimba wimbi, nenda chombo!
Dhoruba ime'sha anza! Na yote yaliyobaki
Ni ya kufa na kupona.

BURUTO: Ho, Lusilio, sikia! Hebu tuseme kidogo.

LUSILIO: Bwana wangu? (*Buruto na Lusulio wanazungumza kando*)

KASIO: Messala!

MESSALA: Jemadari kaniita;—nini jemadari wangu?

KASIO: Messala, leo ni siku yangu niliyozaliwa:
Kasio alizaliwa siku kama hii leo.
Lete mkono, Messala: kuwa ni shahidi wangu
Ya kwamba bila utashi wangu nimelazimishwa,
Vile vile kama Pompe, kufanya pigano moja
Ndilo liwe tegemeo la uhuru wetu wote.
Unajua Epikuro nilimheshimu sana
Pamwe na mafunzo yake; sasa nimebadilika,

Na kuanza kuamini mambo ya ndege wabaya.
Tulipokuwa tukija tukitoka Sardisi,
Tai wakubwa wawili walikuja wakatua
Juu ya bendera yetu ya mbele wakalafua
Na kushiba mikononi mwao askari wetu:
Na wakatufuatia hadi na hapa Filippi.
Wameruka asubuhi ya leo na kwenda zao;
Na badala yao sasa kunguru na kina mwewe
Wanaturuka vichwani kwetu na kuchungulia
Kama kwamba tulikuwa mawindo yao dhaifu.
Vivulivyo vinakuwa kama mwamvuli wa baa,
Ambao kwa chini yake jeshi letu limekaa,
Langoja kukata roho.

MESSALA: Usiyaamini hayo.

KASIO: Naamini nusu nusu; ninao moyo thabiti
Na nimesha kunuia kupambana na hatari
Zote kishujaa hasa.

BURUTO: Sawasawa, Lusilio.

KASIO: Na sasa, Buruto bora, miungu inatupenda,
Ili nasi kirafiki, wenzi katika amani,
Twendelee vivyo hivyo hadi katika uzee!
Lakini mambo ya watu kwamba hayana hakika
Ni heri tufikirie yawezayo kutokea.
Iendapo tukashindwa katika pambano hili,
Basi hii itakuwa ni mara yetu ya mwisho
Kuzungumza pamoja: wewe utafanya nini?

BURUTO: Hata kwa sheria ile ya imani ilofanya
Nikamlaumu Kato kwa kifo alichojipa,
Sijui vipi, lakini naona kuwa ni woga
Na uovu, kwa kuhofu yawezayo kutokea,
Mtu kufupisha hivyo muda wake wa uhai.
Tajipatia silaha ya subira ningojee
Maongozi ya uweza fulani wa huko juu
Ambao watutawala sisi tulo hapa chini.

KASIO: Basi, kama tukishindwa katika pigano hili,
Utakubali ushikwe mateka ukatembezwe
Kwa ushujaa katika mabarabara ya Roma?
BURUTO: La, hasha, Kasio, hasha: siwaze Mrumi bora,
Ati Buruto aweza kwenda Roma amefungwa;
Ana moyo mkubwa mno. Bali siku hii hii
Haina budi ilete mwisho wa shughuli ile
Iloanzwa na tarehe ya katikati ya Machi,
Na sijui kama tena twaweza tukakutana.
Basi buriani yetu ya milele ipokee:
Kwa milele na milele, ni buriani, Kasio!
Endapo tukakutana basi, tutafurahika;
Tusipokutana tena kwa heri hii ni sawa.
KASIO: Kwa milele na milele, ni buriani, Buruto!
Endapo tutakutana tutafurahi hakika;
Bali tusipokutana kwa heri hii ni sawa.
BURUTO: Haya, basi, tangulia, Laiti mtu angeza
Kufahamu na mapema mwisho wa shughuli hii,
Kabla mwisho wenyewe haujawadia bado!
Bali yatosha kujua kuwa siku itakwisha,
Na hapo mwisho wenyewe pia utajulikana!
Haya, na tuende zetu!

Onyesho la II: Mbugani kule kule penye mapigano

(*Tarumbeta: Buruto na Messala wanaingia*)

BURUTO: Kimbia, hima, Messala, yape karatasi hizi
Majeshi ya ng'ambo ile: na yashambulie mara,
Maana`naona kuwa upande wa Ottavio
Hauna moyo thabiti, shambulio la ghafla,
Litawafuta kabisa. Haya, kimbia, Messala:
Wote na watelemke.

Onyesho la III: Sehemu nyingine ya mbuga

(*Tarumbeta: Kasio na Titinio wanaingia*)

KASIO: O, tazama, Titinio, washenzi wanakimbia!
Nimekuwa ni adui wa mtu wangu mwenyewe.
Huyu mshika bendera alitaka kukimbia,
Nikamwua mwoga huyu na kuchukua bendera.
TITINIO: Loo, Kasio, Buruto aliharakisha mno;
Alikuwa na nafuu kumzidi Ottavio,
Akaifanyia pupa: basi askari wake
Wakavutwa kwa mateka na huku tumezungukwa,
Na Mariko Antonio.

(*Aingia Pindaro*)

PINDARO: Kimbia mbali, bwanangu, kimbilia mbali sana
Mariko Antoni yuko kambini kwako, bwanangu:
Kwa hiyo, Kasio bora, kimbia mbali zaidi.
KASIO: Papa hapa kilimani ni umbali wa kutosha.
Ona, ona, Titinio, kule nionako moto
Ni katika kambi yangu?
TITINIO: Naam, ndiko, bwana wangu.
KASIO: Titinio, wanipenda? Mpande farasi wangu,
Umwendeshe kwa haraka mpaka akakufikishe
Kunako majeshi yale, na kisha akurudishe;
Ningependa nifahamu ikiwa majeshi yale,
Ni majeshi ya rafiki au ni ya maadui.
TITINIO: Nitarudi sasa hivi. (*Anaondoka*)
KASIO: Nenda, Pindaro, kapande juu ya kilima kile;
Macho yangu si mazuri; mwangalie Titinio,
Unambie uonayo kule kwenye tambarare.

(*Pindaro anapanda kilima*)

Siku kama hii ndiyo nilianza kupumua:
Wakati umezunguka na kurudi nyuma tena,
Pale nilipoanzia ndipo nifa'poishia;
Dira ya maisha yangu sasa imekamilika.

Je, habari gani, wee?
PINDARO: (*Juu*) O, bwana wangu!
KASIO: Habari gani?
PINDARO: Titinio kazingwa na askari wa farasi,
Wamfuatao kasi; ila anazidi kwenda.
Sasa wamkaribia. Sasa, sasa, Titinio!
Sasa wengine washuka. O, yeye pia kashuka!
Amekwisha kukamatwa. (*Kelele*) Wanashangilia sana.
KASIO: Telemka, njoo chini, usitazame zaidi.
O, mwoga mkubwa mimi, kuishi mpaka kumwona
Rafiki yangu mpenzi ashikwa usoni pangu.
(*Pindaro atelemka*)
Njoo hapa, wee, njoo: nilikuteka Pathia;
Na nilipokunusuru nilikwapisha ya kuwa,
Lotė nitalokwamuru utajaribu kufanya.
Haya, sasa kuwa huru; timiza kiapo chako;
Na kwa upanga mzuri huu ulioingia
Tumboni mwa Kaizari lisafishe tumbo hili.
Usingoje kunijibu: haya, we shika kipini,
Na nitapojifunika uso kama hivi sasa,
Wewe ongoza upanga. (*Pindaro anamchoma*)
Umesha lipa kisasi, Kaizari, tena, basi,
Kwa upanga ule ule uliokuua wewe (*Anakufa*).
PINDARO: Hivi, nimekuwa huru; ila kwa hiari yangu,
Nisingalikuwa huru kwa kupita njia hii.
Loo, Kasio, Pindaro atakimbilia mbali,
Tena ambako Mrumi hatamwona asilani.
(*Anatoka*)
(*Titinio na Messala wanarudi*)
MESSALA: Ni badala, Titinio; kwani Ottavio naye
Ameshindwa na majeshi ya mtukufu Buruto,
Antoni alivyoshinda majeshi yake Kasio.
TITINIO: Kasio atatulizwa sana na habari hizi.
MESSALA: Yeye ulimwacha wapi?

TITINIO: Hapa hapa kilimani, na mja wake Pindaro,
Kalemewa na huzuni.
MESSALA: Je, siye yule ambaye amelala pale chini?
TITINIO: Halali kama yu hai. Maskini, moyo wangu!
MESSALA: Siye yule?
TITINIO: La, siye yule, Messala; ni yule aliyekuwa;
Bali Kasio mwenyewe hapo tena duniani.
O, jua linalokuchwa, uingiavyo gizani
Kwa mionziyo myekundu, vivyo hivyo na Kasio,
Kwa damu yake nyekundu, ndivyo alivyokuchwa.
Jua limekuchwa Roma. Nuru yetu imekwenda.
Sasa mawingu, umande na mashaka vinakuja.
Kazi yetu imekwisha. Shuku ya ushindi wangu
Imetenda tendo hili.
MESSALA: Shuku ya ushindi mwema imetenda tendo hili.
O, ibilisi Mashaka, mtoto wa Kufa Moyo,
Kwa nini wazionyesha akili safi za watu
Mambo yasiyo ya kweli? Ewe mimba ya Mashaka,
Daima wewe huzai mwana wa kufurahisha
Bila kumwua mamako aliyekuzaa wewe!
TITINIO: Kuna nini, we Pindaro! Uko wapi, we Pindaro?
MESSALA: Mtafute, Titinio, nami nende kumlaki
Mheshimiwa Buruto nimchome masikio
Kwa habari mbaya hii. Nina haki ya kusema,
'Nimchome', kwa sababu upanga mkali sana,
Na mishale yenye sumu vyaweza kupokelewa
Sikioni mwa Buruto atakavyozipokea
Habari za afa hili.
TITINIO: Haraka Messala, nami tamtafuta Pindaro.
(*Messala anatoka*)
Kwa nini ulinitaka nije, Kasio shujaa?
Je, siyo rafiki zako niliokutana nao?
Na si wao walonipa shada hili la ushindi,
Na kunambia nikupe? Hukuwasikia shangwe?

Ole wangu, kila jambo ulielewa vibaya!
Lakini, basi, livae shada hili shingonimwo;
Nilitumwa na Buruto wako nikuleteelo,
Na mimi nitatimiza kama alivyoagiza.
Buruto, njoo haraka, ujionee mwenyewe
Nilivyomheshimuye Bwana Kayusi Kasio.
Kunradhini, miungu. Ndiyo haki ya Mrumi.
Njoo, singe ya Kasio, njoo uutafute
Moyo wake Titinio.

(*Anajiua*)

(*Tarumbeta: Messala anarudi pamoja na Buruto, Kato mdogo, Stirato, Volumnio na Lusilio*)

BURUTO: Wapi, ni wapi, Messala, yalipo maiti yake?
MESSALA: Lo, kule; na Titinio yuko anayalilia.
BURUTO: Titinio yuko chali; uso wake uko juu.
KATO: Kauawa.
BURUTO: O, ungali na uwezo, Juliasi Kaizari!
Roho yako yazunguka ko kote na kuzifanya
Panga zetu ziingie matumbo yetu wenyewe.

(*Tarumbeta kidogo*)

KATO: A, Titinio shujaa! Ona, kamvisha taji,
Na marehemu Kasio!
BURUTO: Hivi bado wangalipo Warumi wawili hai,
Walio sawa na hawa? Mrumi wa mwisho, kwa heri!
Roma haiwezi kamwe kuzaa kifani chako.
Rafiki zangu wapenzi, nawiwa machozi mengi
Naye marehemu huyu kuliko mtavyoweza
Kuniona nikilipa. Tapata saa, Kasio,
Tajipatia wasaa. Haya, basi pelekeni
Maiti yake Thasosi: mazishi hayatakuwa
Katika makambi yetu, isije tuua moyo.
Haya, Lusilio njoo; na kijana Kato, njoo;
Twendeni zetu mbugani. Labeo na Fulavio,
Pangeni majeshi yetu. Ni saa tisa, Warumi;

Na kabla ya usiku tutajaribu bahati
Kwenye pigano la pili.

(*Wanatoka*)

Onyesho la IV: Sehemu nyingine ya mbuga

(*Tarumbeta: wanaingia wakipigana Askari wa majeshi yote mawili: halafu, Buruto, Kato mdogo, Lusilio na wengine*)

BURUTO: Bado wananchi, bado, jipigeni moyo konde!
KATO: Ni mwana haramu gani, huyo ambaye hawezi?
Nani atanifuata? Mimi nitalitangaza
Jina langu mbuga nzima: ndimi mwana wa Kato, ho!
Adui wa madhalimu, rafiki wa nchi yangu;
Mimi ndiye mwana wa Mariko Kato, haya, haya!

(*Anashambulia adui*)

BURUTO: Na mimi ndiye Buruto, Mariko Buruto mimi;
Rafiki wa nchi yangu; nijueni ni Buruto.

(*Anatoka na kushambulia adui: Kato anashindwa na kuanguka*)

LUSILIO: Oo, mtukufu kijana Kato, umetupwa chini?
Sasa wafa kishujaa kama vile Titinio;
Tena utaheshimiwa ipasavyo bin Kato.
ASKARI 1: Jitolee, au wafa!
LUSILIO: Nitajitolea nife:
Kuna cha kutosha hapa uniue mara moja;

(*Anampa fedha*)

Jipatie utukufu kwa kumuua Buruto.
ASKARI 1: La, hasha hatuthubutu – Ni mateka mtukufu!
ASKARI 2: Haya! Mwambie Antoni kuwa Buruto katekwa
ASKARI 1: Nitapeleka habari:.– Jemadari huyu aja.

(*Antonio anaingia*)

Buruto amesha shikwa, Buruto kashikwa, bwana.
ANTONIO: Yuko wapi?

LUSILIO: Yu salama, Antonio; yu salama salimini:
Nathubutu kukwambia kuwa hapana adui
Atoweza kumshika Buruto bora mzima:
Miungu watamwepusha na fedheha kama hiyo!
Hapo utapomkuta, awe kafa au hai,
Atakutwa ni Buruto, kama alivyo mwenyewe.
ANTONIO: Siye Buruto, rafiki, walakini nakwambia,
Na huyu pia ni tuzo la thamani ile ile:
Mlindeni mtu huyu, atendewe kila jema:
Napenda watu kamaye kuwa ni rafiki zangu,
Kuliko kuwa adui. Hebu nenda katazame,
Kama Buruto yu hai au kama amekufa;
Halafu lete habari hemani kwa Ottavio,
Mambo yalivyotokea.
(*Wanatoka*)

Onyesho la V: Sehemu nyingine ya mbuga

(*Wanaingia Buruto, Daridanio, Kilito, Stirato na Volumnio*)

BURUTO: Njoni hapa masalia ya rafiki,
Njoni mjipumzishe hapa kwenye jiwe hili.
KILITO: Statilio alionya mwenge; ila hakurudi:
Ikiwa hakukamatwa, basi kauawa, Bwana.
BURUTO: Kaa kitako, Kilito: neno hasa ni kuua;
Ndicho kitendo cha fani. Hebu sikia, Kilito.—
(*Anamnong'oneza*)
KILITO: Nini, mimi, bwana wangu? Katu haiwezekani,
Japo kwa dunia nzima.
BURUTO: Kimya, basi! Usiseme.
KILITO: Afadhali nijiue.
BURUTO: Sikia Daridanio – (*Anamnong'oneza*)
DARIDANIO: Mimi! tendo kama hilo?
KILITO: O, Daridanio!

DARIDANIO: O, Kilito!
KILITO: Ombi gani la maovu Buruto alokuomba?
DARIDANIO: Ati nimwue, Kilito. Ona anatafakari.
KILITO: Chombo kitukufu kile sasa kimejaa ghamu,
Mpaka inafurikia hata kwenye macho yake.
BURUTO: Volumnio mpole njoo, nikwambie neno.
VOLUMNIO: Bwana wangu asemaje?
BURUTO: Ni hivi, Volumnio, mzuka wa Kaizari
Sasa umenitokea mara mbili kwa usiku:
Ya kwanza ni Sardisi; ya pili jana usiku,
Ulinitokea hapa kwenye mbuga za Filippi:
Najua ya kuwa saa yangu sasa imefika.
VOLUMNIO: La, si hivyo, bwana wangu.
BURUTO: Naam, nina hakika imefika, Volumnio.
Waona Volumnio, dunia inavyokwenda; (*Tarumbeta*)
Adui wametusaka mpaka kufikia shimo;
Ni bora humo shimoni tujitupemo wenyewe,
Kuliko kungojelea waje watusukumize.
Volumnio mpole, wajua sisi wawili
Tulisoma shule moja. Kwa hayo mapenzi yetu
Ya zamani, nakusihi, unishikie kipini
Cha upanga wangu huu, na mimi nitajichoma.
VOLUMNIO: Hiyo, bwanangu, si kazi ya kufanywa na rafiki.
(*Tarumbeta*)
KILITO: Kimbia, bwana, kimbia; hapa si pa kuchelewa.
BURUTO: Kwa herini – wewe, wewe na wewe, Volumnio.
Stirato, muda wote ulikuwa umelala;
Nawe, kwa heri, Stirato. Wananchi, moyo wangu
Unafurahika kwamba maishani mwangu mwote
Kamwe sikukuta mtu aso mwaminifu kwangu.
Siku ya kushindwa hii itanipa utukufu,
Kuzidi wa Ottavio na Mariko Antonio,
Watakaojipatia kwa ushindi mwovu huu.

Basi, kwa herini kwani ulimi wake Buruto
Karibu utamaliza ngano ya maisha yake.
Sasa usiku wa giza walemea macho yangu;
Na mifupa yangu nayo, ilofanya kazi kubwa,
Kufikia saa hii yataka kupumzika.
(*Tarumbeta: Kelele ndani*, 'Kimbia! Kimbia! Kimbia')
KILITO: Kimbia, bwana, kimbia!
BURUTO: Haya! Nitafuatia.

(*Kilito, Daridanio na Volumnio wanatoka*)

Nakusihi, Stirato, wewe mhani bwanao.
Wewe ni mtu ambaye unayo heshima bora;
Maishayo yamepata kuuonja utukufu;
Basi, shika sime yangu, na utazame kwingine,
Na mimi nitajichoma. Utaweza, Stirato?
STIRATO: Lete kwanza mkonowo; buriani, bwana wangu.
BURUTO: Kwa heri, Stirato mwema. Kaizari, sasa poa:
Sikukwua kwa nusu ya nia njema kama hii.

(*anajiua*)

(*Tarumbeta: Wanaingia Ottavio, Antonio, Messala Lusilio, na Jeshi*)

OTTAVIO: Yule, kule mtu gani?
MESSALA: Ni mtu wa bwana wangu. Stirato, bwanao wapi?
STIRATO: Yu salama na utumwa ulimo wewe, Messala:
Washindi wanachoweza ni kumchoma moto tu;
Kwani Buruto mwenyewe amekwisha kujishinda.
Na hako mtu mwingine mwenye sifa ya kumwua.
LUSILIO: Hivyo ndivyo ipasavyo Bwana Buruto kukutwa.
Nakushukuru Buruto, kwa kuthibitisha kuwa
Alosema Lusilio yalikuwa ni ya kweli.
OTTAVIO: Watu wote walokuwa watumishi wa Buruto
Mimi nitawachukua. Wewe, utakuja kwangu?
STIRATO: Naam, kama Messala atanikabidhi kwako.
OTTAVIO: Mwambie, Messala mwema.
MESSALA: Bwanangu alikufaje; Stirato?

STIRATO: Nilimshikia sime, akajichoma mwenyewe.
MESSALA: Basi sasa, Ottavio, mchukue awe wako,
Alompa bwana wangu huduma yake ya mwisho.
ANTONIO: Huyu ndiye alikuwa Mrumi bora wa wote:
Mahaini wale wote, kumwondoa peke yake,
Walitenda walotenda kwa sababu ya husuda,
Waliyomhusudia mtukufu Kaizari;
Ila yeye peke yake, kwa nia safi kabisa,
Na kwa faida ya umma, akawa mmoja wao.
Alikuwa mwadilifu mwenye maisha manana;
Na vipaji vilikuwa vimechanganyika kwake,
Miungu wangaliweza kusimama na kusema,
Kwa ulimwengu mzima, 'Huyu alikuwa mtu!'
OTTAVIO: Basi na tumtendee sifa yake ipasavyo,
Kwa heshima na kanuni zinazopasa mazishi.
Na leo maiti yake yalale hemani kwangu,
Yatendewe kwa heshima ipasavyo askari.
Basi wapumzisheni askari wa mbugani,
Na tukagawe neema za siku ya heri hii.

(*Wanaondoka*)

Katika toleo hili la pili, likilinganishwa na lile la kwanza, mna mabadiliko mengi. Makosa madogo madogo yaliyopenyapenya katika toleo la kwanza humu yamesahihishwa; walakini badiliko kubwa ni kwamba majina yamefanywa yatamkike Kiswahili, na hili limesababisha kufanywa mabadiliko mengi kidogo katika ile mistari ambamo mna majina hayo.

Mabadiliko haya yatawawezesha wale wanaosema Kiswahili kuuigiza mchezo huu kwa urahisi zaidi kwa sababu mapigo ya maneno yake hayaharibiki kwa kuingiliwa na majina ya kigeni yaliyo na muundo tofauti.

Mwalimu Julius K. Nyerere vile vile amemaliza kuufasiri mchezo mwengine wa Shakespeare uitwao *The Merchant of Venice*. Nao umepigishwa chapa kwa jina la *Mabepari wa Venisi*.

OXFORD UNIVERSITY PRESS
EAST AND CENTRAL AFRICA

ISBN 0 19 572169 1